**(Operation Tribulation Rescue – Swahili, 20 March 2017)**

**([www.tribulationrescue.com](http://www.tribulationrescue.com) )**

**20 Machi 2017**

OPERESHENI YA KUWAOKOA KUTOKA KWENYE DHIKI

ILANI YA KURUDI KWA YESU

KUJIHAMI KWA WATAKAOACHWA NYUMA

UINJILISTI KOTE DUNIANI


1. Ukurasa wa kuanzia
2. Ni jinsi gani nitakavyookoka?
3. Nimeokoka…ni nini sasa?
4. Dhiki kuu na mwongozo wa uokoaji- mamilioni watoweka….kwa nini?
5. Matukio ya siku za mwisho
6. Tunachoamini
7. Ukweli kutoka katika biblia
8. Mambo ya kimsingi kutoka kwenye biblia
9. Rasilimali zinazopendekezwa
10. Maono na malengo
11. Kuhusu sisi
12. Wasiliana/jiunge nasi

# 1. Ukurasa wa kuanzia

**Matukio kumi na mawili ya siku za mwisho yatakayoibadilisha dunia!**

Ni Mungu pekee anayefahamu na kujua kuhusu wakati mfululizo wa matukio ya siku za mwisho utaanza.

Ilani/Onyo!

Mamilioni ya watu watakapotoweka, utahitaji kuokolewa.

1. Kutoweka kwa mamilioni ya watu (Unyakuzi wa Wakristo)
2. Kutengenezwa kwa Himaya moja ya Ulimwengu (Babeli MKuu)
3. Mataifa kushambulia Israeli…Mungu kuyaangamiza mataifa hayo
4. Mkataba wa Amani kati ya Israeli na Mpinga Kristo. (Mwanzo wa dhiki kuu)
5. Manabii wawili katika Israeli (Nguvu za Kipekee)
6. Kujengwa tena kwa Hekalu la Kiyahudi Yerusalemu.
7. Mapigo Ishirini na Moja ya Mungu. (Vifo vya Mabilioni)
8. Kuuawa kwa Mpinga Kristo (Kufufuka kutoka kwa wafu)
9. Mpinga Kristo kuvunja agano….Unajisi wa Hekalu
10. Kuuawa kwa manabii wawili (Kufufuka kutoka kwa wafu)
11. Chapa ya Mnyama kuhitajika.
12. Ujio wa Yesu Kristo (Siku ya Hukumu).

**WAPASWA KUFANYA NINI?**

**Okoka**

Eneza habari njema kuhusu Yesu Kristo.

Soma mwongozo wa kuwaokoa kutokana na dhiki.

(kwa habari zaidi rejelea matukio ya nyakati za mwisho na unabii wa Biblia wa nyakati za mwisho)

## 2. Ni Jinsi Gani Nitakavyookoka?

Je, unajua kuwa Biblia ina habari mbaya na habari njema! Habari mbaya ni kitu kinachokuhusu wewe. Habari njema ni kitu kinachohusu Mungu.

Ebu tuangazie habari mbaya kwanza.

**HABARI MBAYA**

1) Twahitaji Yesu Kristo ili tusipotee kwa kuwa kila mtu ni mwenye dhambi. “Kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.” (Warumi 3:23)
2) Adhabu ya dhambi ni kifo. “Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu bwana wetu.” (Warumi 6:23)

**HABARI NJEMA**

1) Yesu anakupenda. Alikufa kwa ajili yako na akafufuka. (alilipa adhabu ya dhambi zako). “Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa tungali wenye dhambi.” (Warumi 5:8)
2) Kwa Imani unaweza kuokolewa. “Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako yakuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako yakuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.” (Warumi 10:9)

Swali: Kuna kitu chochote kinachokuzuia kuanzia sasa kumuamini Kristo ndiye mwokozi wako?

**Sala iliyopendekezwa.**

Ewe Mwenyezi Mungu, ninakuja kwako sasa. Najua kuwa mimi ni mwenye dhambi. Naamini Yesu Kristo alikufa kwa ajili yangu na akafufuka. Sasa hivi namuamini Yesu Kristo kama mwokozi wangu. Asante kwa msamaha na uzima wa milele nilionao sasa.Kwa jina la Yesu. Amina.

Ikiwa umeweka tumaini lako kwa Yesu Kristo, Hongera na karibu kwenye familia ya Yesu Kristo Dhambi zako zote zimesamehewa na sasa unauzima wa milele katika Yesu Kristo ambao kamwe hauwezi kuchukuliwa kutoka kwako. Hiyo inammanisha wokovu na usalama wa milele unategemea ukweli wa neno la Mungu sio hisia.

Wokovu hautegemei matendo yako mema. “Kwa maana mmeokolewa kwa neema kwa njia ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu wala si kwa matendo awaye yote asije akajisifu.” (Waefeso 2:8-9)

Kariri mistari hii yote ya wokovu kwa haraka iwezekanavyo ili uweze kushiriki na wengine kujihakikishia wokovu wako mwenyewe.

**Uhakika wa Uzima wa milele.**

Uhakika wa wokovu umeonyeshwa wazi katika maandiko.Ukishaokoka umeokoka kila wakati kwakuwa wokovu wetu unategemea kabisa imani na kile Kristo alitufanyia, hii inamaanisha kuwa hakuna kitu unachoweza kufanya ambacho kitasababisha kuachilia wokovu wako. Huo ni uhuru wa kweli katika Kristo.

**Yohana 5:24** “Hakika nawaambia, yeye alisikiaye neno langu na kumuamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele wala haingii hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.”

**1 Yohana 5:13** “Nimewaandikia nyinyi mambo haya ili mjue yakuwa mnauzima wa milele ninyi mnaloliamini jina la mwana wa Mungu.”

**Yohana 3:16-17** “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wa pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma mwanawe ulimwenguni ili ahukumu ulimwengu bali ulimwengu uokolewe kupitia yeye.”

**Vifungu zaidi vya Biblia**

- **Matendo 16:31** "……mwamini bwana Yesu, nawe utaokoka."
- **Yohana 20:31** "Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini yakwamba Yesu ndiye Kristo Mwana wa Mungu na kwa kuamini muwe na uzima kwa jina lake."
- **Yohana 14:6** "Yesu kamwambia mimi ndie njia ya ukweli na uzima. Mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi."
- **Warumi 1:16,** "Kwa maana sionei haya injili ,kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila amiiniye ,kwa magaidi kwanzo na kwa ngunami pia."
- **2 Wakorintho 5:17,** "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; yakale yamepita tazama! Yamekuwa mapya."
- **Waefeso 1:13-14,** "Nanyia pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu, tena mmekwisha kumuamini yeye na kutiwa chapa na roho Yule wa ahadi aliye mtakatifu, ndiye aliye arabuni ya uridhi wetu ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa utukufu wake."
- **Yohana 3:36,** "Amwaminie bwana yuna uzima wa milele, asiyemwamini bwana hataona uzima bali ghadhabu ya Mungu inamkalia."
- **Matendo 4:12,** "Wala hakuna wokovu katika mwengine awaye yote kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo."
- **Tito 3:5-6** "Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi bali kwa rehema yake kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na roho mtakatifu. Ambaye alitumwagia kwa wingi kwa njia ya Yesu christo mwokozi wetu."
- **Yohana 1:12,** "Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu hatua inayofuata, nenda, nmeokoka… nini sasa?"

Kwa habari zaidi juu ya wokovu na kukua katika Bwana, nenda kwa: **Rasilimali zinazopendekezwa**

Kwa hatua inayofuata, nenda Kwa: **Nimeokoka … ni nini sasa?**

## 3. Nimeokoka … ni nini sasa?

Sio lazima usubiri hadi uwe umesoma Biblia yote kabla ya kwanza kumtumikia Bwana na kushiriki imani yako. Baada ya mtume Paulo kuokoka mara moja alianza kumtangaza Yesu katika Sinagogi (Matendo 9:20). Mungu atakupa nguvu na ujasiri unayohitaji na maneno yakusema shirikini kile Yesu amekufanyia kutoka moyoni mwako. Muulize bwana jinsi anaweza kukutumia kwa heshimia na utukufu wake.

**OMBA**

"Furahini siku zote, ombeni bila kukoma, shukuruni kwa kila jambo maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu." (1 Wathesalonike 5:16-18)

"Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani." (Wakolosai 4:2)

"Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidi."  (Yakobo 5:16)

"Ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akaketi usiku kucha katika kumuomba Mungu." (Luka 6:12)

(Warumi 8:26; Waefeso 6:18; Waebrania 4:14-16; 2Mambo ya nyakati 7:14; Wafilipi 4:6-8; Mathayo 6:5-13, 15:36; Marko 1:35; Luka 5:16, 11:1-13)

**Soma Biblia**

Soma Biblia na kukariri neno la Mungu iwezekanavyo. Ikiwa huna Biblia au huwezi kupata, chapisha sehemu za Biblia kutoka kwa wavuti. Kama kweli umeshinikizwa kwa muda, anza kwa kusoma Luka (Kuzaliwa, Maisha, Kifo na Ufufuo wa Yesu), Matendo (Mwanzo wa kanisa na mateso ya waumini), Warumi (Wokovu  kwa Imani ), Mwanzo (Jinsi vyote vilianza), Ufunuo (Jinsi yote yanaisha), Zaburi (hutoa faraja na nguvu).

Ikiwa haukubanwa na muda soma vitabu hapo juu ya Biblia kisha urudi nyuma na usome Agano Jipya lililosalia tangu mwanzo na agano lingine la zamani. Hakuna mbadala wa neno la Mungu kama muumini Roho mtakatifu atakusaidia kuelewa kila unachokisoma, jinsi unaweza kutumia maandiko kwa maisha yako na kutambua kile Mungu anataka ufanye.

(Kumbu kumbu la Torati 6:4-8, 17:19; Yohana 8:31-32; Isaya 55:11;  1 Petro 3:15)

“Neno lako nitaa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu.” (Zaburi 119:105)

“Jitahidi kuonyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, Mtendakazi asiye na sababu ya kutahayari ukitumia kwa halali neno la kweli.” (2 Timotheo 2:15)

“Moyoni mwangu nimeliweka neno lako nisije nikakutenda dhambi.” (Zaburi 119:11)

“Sikurudi nyuma kuacha amri ya midomo yake.Nimeyatunza maneno ya kinywa chake zaidi ya riziki yangu.” (Ayubu 23:12)

“Heri mtu Yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki, wala hakusimama katika njia ya wakosaji wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo na sheria yake huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halianguki na kila alitendalo litafanikiwa.” (Zaburi 1:1-3)

“Neno la Kristo naikae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kwa zaburi na nyimbo, na tenzi za rohoni huku mkimwimbia Mungu kwa nyimbo za rehema mioyoni mwenu.” (Wakolosai 3:16)

**Jiunge na kanisa (kabla ya unyakuo)**

Tafuta kanisa linaloamini Biblia na ubatizwe kama onyesho la imani yako. Kanisa litakuandaa kumtumikia Bwana. Jiunge na kikundi kidogo na ukue katika bwana unapoomba kuabudu na kushirikiana na waumini wengine.

**Jiunge na Kanisa (Baada ya unyakuo)**

Tafuta waumini wengine ili uweze kusali, kuabudu na kukua, kuudumu na kushirikiana pamoja. Tafuta kanisa la nyumbani au anzisha kanisa la nyumbani na ubatizwe kama onyesho la wazi la imani yako. Makundi yote yenye sauti za kibiblia yatakuwa huru. (Au karibu nayo) na mateso dhidi ya wakristo yanaweza kukuzuia kukutana kwenye jengo la kanisa. Kanisa lako la nyumbani litasaidia kukupa ufanisi wa Bwana.

“Natuangalie jinsi tunavyoweza kuchochea kwa upendo na matendo mema,na tusiache kukusanyika pamoja kama wengine wanavyofanya lakini huimizana – na zaidi kama unavyoona siku inakaribia.” (Waebrania 10:25)

“HIVYO Kristo mwenyewe aliwapa mitume,manabii,wainjilisti, wachungaji na walimu kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu hata kazi ya huduma itendeke ata mwili wa Kristo ujengwe hata na sisi tutakapoufikia umoja  wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu hata kuwa mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo.” (Waefeso 4:11-13)

“Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu wakawa wakiudumu katika fundisho la mitume na katika ushirika na katika kuumega mkate na katika kusali.” (Matendo 2:41-42)

**INJILI – ENEZA HABARI NJEMA**

Eneza habari njema kuhusu Yesu Kristo na familia yako na marafiki na wengine wengi kadri uwezavyo.

“Basi nendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi wangu, mkiwabatize kwa jina la Baba la Mwana na la Roho mtakatifu na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru nyinyi na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, ata ukamilifu wa dahari.” (Mathayo 28:19-20)

“Ndivyo ilivyoandikwa kuwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi kuanza tangu Yerusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya.” (Luka 24:46-48)

“Ndipo alipowaambia wanafunzi wake, mavuno ni mengi lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno yake.” (Mathayo 9:37-38)

“Na kila siku, ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo.” (Matendo 5:42)

## 4. Dhiki kuu na mwongozo wa uokoaji- mamilioni watoweka….kwa nini?

Kwa nini mamilioni ya watu walipotea? Yesu amerudi na kuchukua waumini wake wote mbinguni, tukio hili (unyakuo) lilitabiriwa katika Biblia karibu miaka 2,000 iliyopita kwa habari

ya ziada nenda kwenye matukio ya nyakati za mwisho (mamilioni watoweka – unyakuo wa wakristo).Yesu anakuja tena katika miaka michache kuwaokoa waumini wapya, kuwahukumu waovu na kutawala ufalme wake wa kidunia. Tunaomba kwamba uwe mmoja wa waumini hawa wapya. Nenda kwa nawezaje kuokoka? Kujua jinsi ya kuwa muumini wa Yesu.

Sasa kwa kuwa uliachwa nyuma, nyakati ngumu na zenye changamoto ziko mbele. Mabilioni watakufa wakati wa dhiki kuu (miaka saba ndefu) na kwa bahati mbaya unaweza kuwa mmoja wao. Watu wataogopa na kuchanganyikiwa na kutafuta majibu. Utasikia kila aina ya nadharia juu ya kile kinachoweza kutokea kwa mamilioni waliopotea wanaweza kusema kwamba Mungu alihukumu "wasiovumilia" au washirika walituondoa, lakini Biblia inafunua ukweli.

"Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la bwana kwamba sisi tulio hai tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu bwana mwenyewe atashika kutoka mbinguni pamoja na mwaliko na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai tulio salia tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili kumlaki bwana hewani na hivyo tutakuwa pamoja na bwana milele. Basi farijianeni kwa maneno hayo." (1 Wathesalonike 4:15-18)

Lazima umgeukie bwana kushinda hofu yako na wasiwasi na upokee amani na faraja ambayo ni yeye tu anaweza kutoa. "Msijisumbue kwa neno lolote. Bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu ipitayo akili zote itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu. Hatimaye ndugu zangu, mambo yote yaliyo ya kweli yote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema; ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote yatafakarini hayo." (Wafilipi 4:6-8)

Huu sio wakati wa kunywea nyuma kwa hofu, kukabiliana na kujificha. Lazima umuombe Bwana kwa nguvu na ujasiri na amani ambayo yeye peke yake anaweza kutoa lazima uinuke juu ya hali yako ukisukuma kando hofu yako, wasiwasi na mashaka. Yesu Kristo tayari amekuhakikishia ushindi karibu miaka 2000 iliyopita wakati alipoteseka na kufa msalabani na akachukua dhambi za ulimwengu. Kufufuka kwake kutoka kwa wafu kulikuwa thibithisho kwamba alishinda dhambi, kifo na Ibilisi.

Hawana nguvu tena juu yako .Ikiwa kwa sababu huishi dhiki utakuwa maramoja katika uwepo wa Bwana mradi umeamini Yesu Kristo ndiye mwokozi wako. Kuna miaka saba tu iliyobaki (Baada ya mkataba wa amani Waisraeli.) "Kuwafanya wanafunzi wa mataifa yote" Kabla ya Yesu Kristo kurudi kama "MFALME WA WAFALME NA BWANA WA MABWANA" Kuokoa watu wake, kuhukumu waovu na kuutawala ufalme wa kidunia.

Fanya kila wakati kuhesabiwa kwa heshima na utukufu wa Bwana Yesu Kristo. Kunazaidi ya watu bilioni sita wanaohitaji kusikia juu ya Yesu kwa hiyo endelea.Kumbuka tayari tunajua hadithi hii ya wakati wa mwisho inaisha-Yesu anashinda!

Mungu atafanya kazi na njia zake kuu na za nguvu katika siku hizi za mwisho na tunaomba kwamba utashiriki katika mlipuko huu wa injili wa wakati wa mwisho na uamsho mkubwa katika historia ya mwanadamu.

Tunataka ujue kuwa hauko peke yako. Yesu alisema, "….mimi nipo pamoja nanyi siku zote, ata ukamilifu wa dhahari" (Mathayo 28:20). "Unaweza kuwa na hakika kuwa wewe uko katika Bwana na katika uweza wa nguvu zako." (Waefeso 6:10)

**Vipaumbele vyako vya juu ni;**

**Okoka.**

Okoka (Umehakikishiwa msamaha wa dhambi na uzima wa milele) – Tazama- naweza kuokoka? Nimeokoka…Ni nini sasa?

"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako kwa kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako yakuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka." (Warumi 10:9)

"Kwa maana jinisi hii Mungu akaupenda Ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wapekee ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele." (Yohana 3:16)

"Yesu akamwambia, "Mimi ndimi njia na kweli na uzima; Mtu haji kwa Baba ila kwa njia yangu mimi." (Yohana 14:6)

**Omba**

“Furahini siku zote, ombeni bila kukoma shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu” (1 Wathesalonike 5:16-18)

“Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku shukrani” (Wakolosai 4:2)

“Ungameni dhambi zenu nyinyi kwa nyinyi, na kuombeana mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenyehaki kwa faa sana, akiomba kwa bidii” (Yakobo 5:16)

“Ikawa sikuzile Yesu aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumuomba Mungu.” (Luka 6:12)

(Warumi 8:26; Waefeso 6:18; Webrania 4:14-16; 2Mambo ya nyakati 7:14; Wafilipi 4:6-8; Mathayo 6:5-13, 15:36; Marko 1:35; Luka 5:16, 11:1-13)

**Soma Biblia**

Soma Biblia na ukariri neno la Mungu iwezekanavyo. Ikiwa huna Biblia au uwezo kupata chapisho sehemu za Biblia kutoka kwa wavuti.Kama kweli umeshinikizwa kwa muda anza kwa kusoma Luka (Kuzaliwa, Maisha, Kifo na Ufufuo wa Yesu), Matendo (Mwanzo wa kanisa na mateso ya waumini), Warumi (Wokovu kwa Imani ), Mwanzo (Jinsi vyote vilianza), Ufunuo (Jinsi yote yanaisha), Zaburi (kutoa faraja na nguvu).

Iwapo hujabanwa na muda soma vitabu hapo juu vya Biblia kisha urudi nyuma na usome Agano Jipya lililosalia tangu mwanzo na Agano lingine la zamani. Hakuna mbadala wa neno la Mungu kama muumini Roho mtakatifu atakusaidia kuelewa kila unachokisoma, jinsi unaweza kutumia maandiko kwa maisha yako na kutambua kile Mungu anataka ufanye.

(Kumbu kumbu la Torati 6:4-8, 17:19; Yohana 8:31-32; Isaya 55:11; 1 Petro 3:15)

“Neno lako nitaa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu.” (Zaburi 119:105)

“Jitahidi kuonyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, Mtendakazi asiye na sababu ya kutahayari ukitumia kwa halali neno la kweli.” (2 Timotheo 2:15)

“Moyoni mwangu nimeliweka neno lako nisije nikakutenda dhambi.” (Zaburi 119:11)

“Sikurudi nyuma kuiacha amri ya midomo yake.Nimeyatunza maneno ya kinywa chake zaidi ya riziki yangu.” (Ayubu 23:12)

“Heri mtu Yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki, wala hakusimama katika njia ya wakosaji wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo na sheria yake huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halianguki na kila alitendalo litafanikiwa.” (Zaburi 1:1-3)

“Neno la Kristo naikae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kwa zaburi na nyimbo, na tenzi za rohoni huku mkimwimbia Mungu kwa nyimbo za rehema mioyoni mwenu.” (Wakolosai 3:16)

**Jiunge na Kanisa**

Tafuta waumini wengine ili mweze kusali, kuabudu na kukua, kuhudumu na kushirikiana pamoja.Tafuta kanisa la nyumbani na ubatizwe kama onyesho la wazi la imani yako. Makanisa yote yenye sauti za kibiblia yatakuwa tupu (au karibu nayo) na mateso dhidi ya Wakristo yanaweza kukuzuiya kukutana kwenye jengo la kanisa. Kanisa lako la nyumbani litasaidia kukupa ufanisi wa Bwana.

“Natuangalie jinsi tunavyoweza kuchocheana kwa upendo na matendo mema, na tusiache kukusanyika pamoja kama wengine wanavyofanya lakini kuhimizana na zaidi kama unavyoona siku imekaribia.” (Waebrania 10:25)

“Hivyo Kristo mwenyewe aliwapa mitume,manabii,wainjilisti, wachungaji na walimu kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu hata kazi ya huduma itendeke hata mwili wa Kristo ujengwe hata na sisi tutakapoufikia umoja  wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu hata kuwa mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo.” (Waefeso 4:11-13).

“Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu wakawa wakiudumu katika fundisho la mitume na katika ushirika na katika kumega mkate na katika kusali.”(Matendo 2:41-42)

**Injili – Eneza habari njema kuhusu Yesu Kristo**

Eneza habari njema kuhusu Yesu Kristo na watu wengi iwezekanavyo kabla ya Yesu kurudi duniani. (Miaka saba kabla ya mkataba wa amani wa Israeli) Unaweza kuwa sehemu kubwa ya uamrisho mkubwa katika historia ya binadamu.Rudufu habari nyingi kutoka kwa tovuti iwapo huenda ikazimwa. Hifadhi habari kwenye kompyuta tuta barua pepe na ufanye nakala nyingi ama chochote kingine unawezakufanya kisha usambaze kwa watu wengi iwezekanavyo.

“Basi nendeni mkawafanye mataifa yote wanafunzi wangu muwabatize kwa jina la Baba, na mwana na Roho mtakatifu na kuwafundisha kuyashika yote  niliyo waamuru nyinyi, na tazama mimi nipo pamoja nanyi  siku zote  ata ukamilifu wa fahari.” (Mathayo 28:19-20)

“Ndivyoilivyoandikwa kuwa, kwamba Kristo atateswa na atafufuka siku ya tatu na kwamaba mataifa yote yatahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi kuanza tangu Yrusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya.” (Luka 24:46-48).

“Ndipo alipowaambia wanafunzi wake, “mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni bwana wa mavuno, apeleke watendakazi katika mavuno yake.” (Mathayo 9:37-38).

“Na kila siku ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo.” (Matendo 5:42).

Onyo! Msipokee alama ya mnyama. Mwengine watatu akawafuata akisema kwa sauti kuu, “Mtu awaye yote akimsujudu mnyama huyo na sanamu yake na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo wa ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu na mbele za mwanakondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele wala hawana Roho mchana na usiku hao wamsujudio mnyama huyo na sanamu yake na kila aipokeaye chapa ya jina lake.” (Ufunuo 14:9-11). “Akienda malaika wa kwanza akakimimina kitasa chake juu ya nchi; pakawa na jipu baya bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya mnyama huyo, na wale wenye kusujudia sanamu yake” (Ufunuo 16:2) (Ufunuo 13:7; 19:20; 20:4)

## 5. Matukio ya siku za mwisho

Waandishi wamejitahidi kadri wawezavyo kutafsiri neno la Mungu kwa usahihi.

**Kuzaliwa upya Kwa Israeli**

Kuzaliwa upya kwa taifa la Israeli ni kutimiza moja ya hafla iliyotabiriwa sana katika maandiko. Israeli ikawa taifa tena mnamo tarehe kumi na nne Mei 1948.

(Siku ya uhuru, miaka mitano 5708 katika kalenda ya Kiyahudi) Tunaamini ya kwamba kuzaliwa upya kwa Israeli kunaanza kuhesabiwa kwa matukio ya wakati wa mwisho.Kuzaliwa upya kwa Israeli maranyingi kunahusishwa ya kwamba kiroho kwa taifa na uamsho. (Ezekieli 11:14-21, 36:22-38, 37:1-28, 39:25-29) Kwa hukumu ya mataifa (Yoeli 3:1-2, Ezekieli 28:24-26) kwa dhiki kuu, (Yeremia 30:1-11) Kwa utawala wa mfalme Daudi na utawala wa Masihi. Mungu atafanya Agano la amani na Israeli na Daudi atakuwa mfalme wao milele. (Ezekieli 34:24, 37:24-28, Yeremia 30:9, Hosea 3:5)

Masihi (tawi lenye haki) atatawala juu ya watu wote wa ulimwengu. (Yeremia 23:1-8, 33:14-16; Isaya 4:2-6, 11:1-5; 53:2 Zakaria 3:8-9, 6:12:13, Ezekieli 20:33-44; Ufunuo 20:4)

Kuzaliwa upya kwa Israeli – Aya za nyongeza (Isaya 11:11-12, Ezekieli 34:11-16, 38:8, Danieli 9:24-27)

**Mamilioni watoweka – Unyakuo wa Wakristo**

Kwa nini mamilioni ya watu watatoweka? Yesu atarudi na kuwachukua waumini wake na kuenda mbinguni kabla ya dhiki kuu ya miaka saba kuanza. Mabilioni ya watu walioachwa nyuma wataogopa na kuchanganyikiwa.Nadharia nyingi zitapendekezwa kuelezea kutoweka kwao, lakini Biblia inafunua ukweli. Unyakuo ulitabiriwa katika Biblia karibu miaka 2000 iliyopita. (Yohana 14:1-3) (Wafilipi 3:20-21, 2 Wathesalonike 2:1-12, 2 Petro 3:3-18, ufunuo 3:10-11)

“Kwa kuwa twawaambieni hata kwa neno la Bwana, Kwamba sisi tulio hai, tutakao salia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko na sauti ya malaika mkuu na parapanda ya Mungu. Nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza kisha sisi tulio

hai, tulio salia tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili tumlaki Bwana hewani na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.” (1Wathesalonike 4:15-17)

“Angalieni, nawaambia ninyi siri ; Hatutalala sote lakini tutabadilika , kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho;  maana parapanda italia na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu,nasi tutabadilika.” (1 Wakorintho 15:51-52)

“Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye hata malaika walio mbinguni, Wala mwana ila Baba pekeyake. Kwa maana kama vile alivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya gharika watu walivyokuwa wakila na kulewa, wakioa na kuolewa, hata siku ile ilipoingia Nuhu katika safina, wasitambue hata gharika ikaja, likawachukua wote ndivyo itakavyokuwa kuja kwake mwana wa Adamu. Wakati ule watu wawili watakuweko kondeni; mmoja atwaliwa, mmoja ataachwa; Wanawake wawili watakuwa wakisaga, mmoja atwaliwa mmoja aachwa; Kesheni basi kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu.

Lakini fahamuni neno hili, kama mwenye nyumba, angejua ile zamu mwivi atakayokuja, angalikesha,wala asingaliacha nyumba yake kuvunjwa. Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; Kwa kuwa katika saa msiyodhani mwana wa Adamu yuaja. Mtumwa mwaminifu au asiyemwaminifu.” (Mathayo 24:36-44)

“Lakini, ndugu kwa habari ya nyakati na majira, hamna haja niwaandikie, maana nyinyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, kuna Amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula, kama vile utungu umjiavyo mwenye mimba, wala hakika hawataokolewa. Bali ninyi, ndugu, hammo gizani hata siku ile iwapate kama mwivi, Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, wana wa mchana, sisi si wa usiku, wala wa giza. Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe na kuwa na kiasi. Maana walalao usingizi hulala usiku, na pia walewao hulewa usiku. Lakini sisi tulio wa mchana, tuwe na kiasi, hali tukijivika kifuani Imani na upendo, na chepeo yetu iwe tumaini ya wokovu kwa kuwa Mungu hakutuweka kwa hasira yake, bali tupate wokovu, kwa bwana wetu Yesu Kristo; ambaye alikufa kwa ajili yetu ili tuishi pamoja naye kwamba twakesha au kwamba twalala. Basi farijianeni na kujengana kila mtu na mwenzake vile vile kama mnavyofanya.” (1 Wathesalonike 5: 1-11)

Watu wengi waliokolewa baada ya unyakuo. Biblia inaonyesha wazi kwamba wakati wa mwisho watu wengi wataokolewa na wengi watapoteza maisha yao kwa Imani yao kwa Bwana Yesu. Kutakuwa na uamsho mkubwa wakati wa nyakati za mwisho. Kitabu cha Ufunuo kinaelezea umati mkubwa wa waumini mbinguni ambao wametoka kwenye dhiki kuu.

"Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kiti cha enzi, mbele za mwana kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao…Hao ndio wanaotoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya mwana-kondoo…Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hali iliyo yote. Kwa maana huyo mwana kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga naye atawaongoza kwenye chemichemi za majiyenye uhai na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao." (Ufunuo 7:9-17)

Kutakuwa na waumini wengi duniani kwamba mpinga kristo, kiongozi wa ufalme wenye nguvu Zaidi katika historia ya ulimwengu atafanya vitu dhidi ya watu watakatifu wa Mungu wakati wa nusu ya pili ya dhiki. (Ufunuo 13:7; Danieli 7: 21-22) (Yohana 16:2; Ufunuo 6:9-11, 15:2-4, 20:4-6).

**Kutengenezwa kwa Himaya moja ya Ulimwengu (Babeli mkuu)**

Hofu ya kimataifa ambayo huenda ikafuata unyakuo, itakuwa motisha kubwa kwa ulimwengu kuungana na kuunda serikali moja ya ulimwengu ambayo itakuwa Babeli mkuu, himaya ya nyakati za mwisho ikiundwa na falme kumi (mikoa) na kutawaliwa na wafalme kumi (Danieli 7;  Ufunuo 17-18) himaya hii itakuwa na nguvu kupita kiasi na itaitawala dunia yote na kuikanyaga na kuiharibu (Danieli 7:23). Nyakati za mwisho Babeli mkuu ameelezwa kwa njia mbalimbali katika Biblia, yeye ni wa kutisha na mnyama mwenye nguvu kupita kiasi ambaye atakuwa karibu na mmoja na mpinga kristo na shetani wakati wa nusu ya pili ya dhiki kuu. Anaelezewa pia kama mfumo wa dini ya uwongo na kahaba (Ufunuo 17:1-18). Kahaba huyo atawachukia watu wa Mungu. Ataharibu dunia na usherati wake, atakuwa tajiri na mwovu kupita kiasi. "Mwanamke huyo alikuwa amevalia zambarau na nyekundu na alikua aking'aa kama dhahabu, mawe ya thamani na lulu. Alikua ameshika kikombe cha dhahabu mkononi mwake,

kilichojazwa na machukizo na uchafu wa uzinzi wake. Jina lililoandikwa kwenye kipaji cha uso wake lilikuwa siri: BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA WA MACHUKIZO YA DUNIA." (Ufunuo 17: 4-5).

Babeli mkuu pia itakuwa jiji kubwa linalotawala juu ya wafalme wa dunia (Ufunuo 17:18). Itakua "makao ya mashetani na makao kwa kila roho chafu" (Ufunuo 18:2). Wafanyabiashara wa dunia watakua matajiri kwa sababu ya anasa nyingi na mataifa yote watakunywa divai yake ya wazimu na wazinzi wake (Ufunuo 14:8, 18:3). Wale wote walio na meli baharini watakuwa matajiri kupitia utajiri wake (Ufunuo 18: 17-19).

Babiloni mkubwa atawajibika kwa mateso na kiso cha waumini wengi na atapata ghadhabu kali ya Mungu, kwa sababu dhambi zake zimerundikwa mbinguni. "Atalewa na damu ya watu watakatifu wa Mungu, damu ya wale waliotoa ushuhuda kwa Yesu," na Mungu atakumbuka uhalifu wake (Ufunuo 16:19, 17:6, 18:4-8). "Kwa sababu hiyo mapigo yake yatakuja katika siku moja, mauti, na huzuni, na njaa, naye atateketezwa kwa moto. Kwa maana Bwana aliyemuhukumu ni mwenye nguvu." (Ufunuo 18:8).

**Mataifa kushambulia Israeli … Mungu ayaangamiza mataifa hayo**

Gogu (Inahusu Urusi) na mataifa mengi yatashambulia Israeli na kikosi kikubwa. Vita hivi pengine hufanyika muda mfupi baada ya unyakuo na inafuatwa na mkataba wa Amani wa Israeli – mpinga Kristo. Ezekieli 38 na Ezekieli 39 yaelezea shambulio hili na jinsi Mungu anavyowaokoa watu wa Israeli kimiujiza. Hukumu ya Bwana wakati wa vita vya Ezekieli 38 itakuwa mojawapo ya maonyesho ya kushangaza ya nguvu za Mungu ambazo ulimwengu umewahi kuona. Matokeo ya tukio hili muhimu sana ya nyakati za mwisho ni kwamba mataifa yatajua kwamba Mungu mwenyezi ni Bwana, yule mtakatifu katika Israeli naye atatukuzwa na jina lake takatifu litajulikana katikati ya watu wake wa Israeli, watu wengi watapata fursa ya kuokolewa kwa kumuamini Bwana Yesu kabla ya dhiki kuu kuanza.

"Nawe utapanda juu uwajilie watu wangu, Israeli, kama wingu kuifunika nchi, itakuwa katika siku za mwisho nitakuleta upigane na nchi yangu, ili mataifa wanijue, nitakapotakaswa kwako, ewe Gogu, mbele ya macho yao." (Ezekieli 38:16).

“Itakuwa katika siku hiyo Gogu atakapokuja kupigana na nchi ya Israeli, asema Bwana Mungu, ghadhabu yangu itapanda katika mianzi ya pua yangu. Kwa maana katika wivu wangu, na katika moto wa ghadhabu yangu, nimenena, Hakika katika siku ile kutakuwako tetemeko kubwa katika nchi ya Israeli. Hata samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama wa kondeni, na vitu vyote vitambaavyo juu ya nchi na wanadamu wote walio juu ya uso wa nchi watatetemeka mbele ya uso wangu; nayo milima itatupwa chini, na magenge yataanguka, na kila ukuta utaanguka chini. Name nitaita upanga uje juu yake katika milima yangu yote, asema Bwana Mungu; nao upanga wa kila mtu utakua juu ya ndugu yake. Name nitamuhukumu kwa tauni, na kwa damu, name nitanyesha mvua ifurikayo, na mvua ya mawe makubwa sana, na moto wa kiberiti juu yake, na vikosi vyake, na watu wa kabila nyingi walio pamoja naye. Name nitajitukuza na kijitakasa, na kujidhiirisha, mbele ya macho ya mataifa mengi; nao watajua ya kuwa mimi ndimi Bwana.” (Ezekieli 38:18-23).

“Utaanguka juu ya milima ya Israeli, wewe na vikosi vyako vyote, na watu wa kabila nyingi walio pamoja nawe, name nitakutoa na kuwapa ndege wa kila namna walao nyama, na wanyama wa nchi, uliwe na wao. Utaanguka katika uwanda; kwa maana mimi nimenena neno hili, asema Bwana Mungu.  Nitapeleka moto juu ya Magogu; na juu ya watu wote wakaao salama katika visiwa; nao watajua ya kuwa mimi ndimi Bwana. Na jina langu takatifu nitalifanya kuwa linajulikana katikati ya watu wangu wa Israeli; wala sitaacha jina langu takatifu kutiwa unajisi tena; nao mataifa watajua ya kuwa mimi ndimi BWANA na aliye mtakatifu katika Israeli. Tazama linakuja nalo litatendeka, asema Bwana Mungu; hii ndiyo siku ile niliyoinena.” (Ezekieli 39:4-8).

**Mkataba wa Amani kati ya Israeli na Mpinga Kristo (mwanzo wa dhiki kuu)**

Kufuatia vita vya Ezekieli 38, utambulisho wa mpinga Kristo hatimaye utajulikana kwa uhakika. Mtu ambaye anafanya mkataba wa Amani wa miaka saba na Israeli atafunuliwa kama mpinga Kristo (Danieli 9:27). Hili ni tukio muhimu sana la wakati wa mwisho kwa sababu kutiwa saini kwa agano pia kutaashiria kuanza rasmi kwa dhiki kuu ya miaka saba.

Mwanzoni mpinga Kristo hatakuwa mmoja wa wafalme kumi wa Babeli mkuu. Danieli anafafanua mpinga Kristo kama pembe ndogo ambayo itatokea wale wafalme kumi, “tofauti na wale wa awali, atawashinda wafalme watatu” (Danieli 7:8, 20, 24). Wafalme waliobaki

wataanguka mmoja baada ya mwengine hadi mpinga Kristo hatimaye atakapokuwa mfalme na mtawala mkuu wa Babeli karibu na dhiki ya katikati. Mpinga Kristo atajaribu kubadilisha nyakati zilizowekwa na sheria, atasema kwa majivuno, ataogopwa, atakuwa na jeraha mbaya na atakuwa hai tena, atafanya vita dhidi ya waumini (kuwatesa na kuwauwa waumini), atajiinua na kujitukuza juu ya miungu wote, atasema mambo yasiyosikiwa juu ya Mungu wa miungu, na ataabudiwa (Ufunuo 13:1-10, 17:1-18, 19:1-21, 20:1-15, 2Wathesalonike 2:1-12; Mathayo 24:15; Danieli 7:7-28, 8:23-26, 9:24-27, 11:36-45, 12:1-13, 1John 2:18-27).

**Manabii wawili katika Israeli (nguvu za kipekee)**

Manabii wawili (mashahidi) watateuliwa na Mungu watabiri kwa siku 1260, wakiwa wamevaa nguo za magunia. Mungu atawapa nguvu maalum. "Na mtu akitaka kuwadhuru, moto hutoka katika vinywa vyao na kuwala adui zao. Na mtu akitaka kuwadhuru hivyo ndivyo impasavyo kuuawa. Hao wana amri ya kuzifunga mbingu ili mvua isinyeshe katika siku za unabii wao. Nao wana amri juu ya maji kuyageuza kuwa damu, na kuipiga nchi kwa kila pigo, kila watakapo." (Ufunuo 11:3-6)

**Kujengwa tena kwa Hekalu la Kiyahudi Yerusalemu**

Ukombozi mkubwa wa Mungu wa watu wake wakati wa vita vya Ezekieli 38 na kushindwa kwa maadui wengi wa Israeli itafungua njia ya ujenzi wa hekalu lililokuwa likingojewa kwa muda huko Israeli. Hekalu litakamilika haraka wakati wa nusu ya kwanza ya dhiki kuu kwa sababu katikati mpinga Kristo atasimamisha kutoa dhabihu na sadaka na kulidhalilisha Hekalu (Danieli 9:27, 12:11; Mathayo 24:15; 2Wathesalonike 2:3-4).

**Mapigo ishirini na moja ya Mungu (vifo vya mabilioni)**

Mabilioni ya watu watakufa wakati wa dhiki kuu. (Ufunuo 6:8, 9:15). "Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingeokoka mtu yeyote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo." (Mathayo 24:22). Hukumu 21 za Mungu ni pamoja na hukumu saba za chapa, hukumu saba za tarumbeta na hukumu saba za bakuli. (Ufunuo 6:1-17, 8:1-13, 9:1-21, 11:15-19, 15:1-8, 16:1-21)

**Chapa saba za hukumu**

Baada ya mkataba wa Amani wa Isaraeli na mpinga Kristo kutakuwa na kipindi kifupi cha amani. Hii itafuatiwa na vita, njaa, mfumuko wa bei uliokithiri, mapigo, kifo cha robo moja ya idadi ya watu duniani, mateso makali ya waumini, matetemeko ya ardhi na usumbufu wa mwezi, jua na nyota (Ufunuo 6:1-17, 8:1-6).

**Hukumu saba za tarumbeta**

Hukumu za tarumbeta ni pamoja na mvua ya mawe na moto uliochanganywa na damu (theluthi moja ya dunia itateketea), nyota kubwa inayowaka inaanguka ikisababisha theluthi moja ya maji safi duniani kuwa sumu, ikifanya giza la jua, mwezi na nyota, nzige/nge wa mapepo, magonjwa na vita (Ufunuo 8:1-3, 9:1-21, 11:15-19)

**Hukumu saba za bakuli**

Katika mapigo hayo saba ya mwisho ghadhabu ya Mungu itakuwa imekamilika (Ufunuo 15:1). Hukumu za bakuli ni pamoja na vidonda vinavyoendelea (inaathiri tu watu walio na alama ya mnyama na wanaoabudu sanamu yake), bahari kuwa damu (maisha yote ya bahari hufa), mito na chemichemi huwa damu, joto kali kutoka kwa jua mto wa Frati hukauka ili kuondoa njia kwa wafalme kutoka mashariki, mapepo hukusanya mataifa yote kwa Har-magedani, tetemeko la ardhi lenye maafa, miji ya mataifa huporomoka, kila kisiwa kinatoweka, milima husawazishwa na mawe ya mvua ya mawe (kilo 45) huanguka juu ya watu (Ufunuo 15-16)

**Kuuawa kwa mpinga Kristo (kufufuka kutoka kwa wafu)**

Mpinga Kristo atauawa na atafufuka kutoka kwa wafu. Shetani (joka) atampa mpinga Kristo (mnyama) nguvu zake na kiti chake cha enzi na mamlaka makubwa kwa nusu ya pili ya dhiki kuu. “Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule. Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa yule mnyama uwezo wake; nao waka msujudu yule mnyama, wakisema, ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye? Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru. Akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili. Akafunua kinywa chake amtukane Mungu na kulitukana jina lake, na maskani yake, nao wakaao mbinguni. Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila ambaye jina lake

halikuandikwa kwenye kitabu cha uzima cha mwana-kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia.” (Ufunuo 13:3-8) (Ufunuo 13:12).

**Mpinga Kristo kuvunja agano (unajisi wa hekalu)**

Mpinga Kristo atavunja mkataba wa Israeli na kudharau hekalu huko Yerusalemu, katikati ya dhiki ya miaka saba (Danieli 9:27; Mathayo 24:15; 2 Wathesalonike 2:3-4). Kwa miaka mitatu na nusu ya wakati wa dhiki kuu, watakatifu wa Mungu watawasilishwa mikononi mwake (Danieli 7:25; Ufunuo 13:5-8).

**Kuuawa kwa manabii wawili (kufufuka kutoka kwa wafu)**

Wakati manabii (mashahidi) wawili watakapomaliza ushuhuda wao huko Yerusalemu, katikati ya dhiki (mnyama (mpinga kristo) atawashambulia na kuwaua wengi wa wakazi wa ulimwengu watasherehekea kifo chao kwa sababu manabii hawa wawili watawatesa wale wanaoishi duniani. Mungu atawafufua kutoka kwa wafu baada ya siku tatu na nusu na watapaa mbinguni katika wingu. Katika saa hiyo kutakuwa na tetemeko kubwa la ardhi mjini Yerusalemu na ushuri ya mji huo itaporomoka na watu elfu saba watauawa. Kwa mujibu wa Malaki, mmoja wa manabii anaweza kuwa Eliya. (Malaki 4:5, Ufunuo 11:3-13).

**Chapa ya mnyama na nabii wa uongo**

Nabii wa uwongo pia anajulikana kama mnyama wa pili na atatumia mamlaka yote ya mpinga Kristo mbele yake. Atafanya ishara kubwa na kuwafanya watu wamwabudu mpinga Kristo na kupokea alama ya mnyama. “Kisha nikaona mnyama mwengine; akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa mwana-kondoo, akanena kama joka. Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona. Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye akawakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya mnyama huyo, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi. Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe. Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa masikini, na walio huru kwa watumwa,

watiwe chapa katika mkono wao wa kuume na katika vipaji vyao vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani jina la mnyama yule au hesabu ya jina lake. Hapa ndipo penye hekima, yeye aliye na akili, na aihesabu hesabu ya mnyama huyo; maana ni hesabu ya kibinadamu. Na hesabu yake ni mia sita, sitini na sita." (Ufunuo 13:11-18). Onyo! Usichukue alama hiyo ya mnyama!

"Na mwengine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, mtu awaye yote akimsujudu mnyama huyo na sanamu yake; na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za mwana-kondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo mnyama huyo na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa la jina lake." (Ufunuo 14:9-11)

"Akaenda huyo wa kwanza, akakimimina kitasa chake juu ya nchi; pakawa jipu baya, bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya mnyama huyo, na wale wenye kuisujudia sanamu yake." (Ufunuo 16:2 Ufunuo 13:7, 19:20, 20:24)

**Ujio wa Yesu Kristo (siku ya hukumu)**

Yesu Kristo, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana anarudi duniani mwishoni mwa dhiki kuu (miaka saba baada ya mkataba wa Amani wa Israeli na mpinga Kristo) kuwaokoa watu wake, kuwahukumu waovu, na kutawala ufalme wake wa kidunia mpinga kristo, wafalme wa dunia na majeshi yao hukusanyika kufanya vita dhidi ya Mungu, mpinga Kristo na nabii wa uwongo walikamatwa na kutupwa maisha katika ziwa la moto la kiberiti kinachowaka na majeshi ya dunia yanaangamizwa. Shetani basi amefungwa kwa miaka elfu moja na kutupwa ndani ya kuzimu. Mataifa yote yatakusanyiwa mbele ya Yesu kwa ajili ya hukumu, wasio waaminifu, "watakwenda kwenye adhabu ya milele lakini wenye haki kwa uzima wa milele." (Mathayo 25:31-46) Ufunuo sura ya 19-20; Isaya 34:1-17, 66:15-17; Danieli 12:1-13; Yoeli 2:28-32; 3:1-17; Zekaria sura ya 12-14, Luka 17:20-37; 2Wathesalonike 1:1-12, 2:1-12; Tito 2:11-14).

Tarehe ya ujio wa Yesu Kristo mara ya pili inaweza kuamuliwa kwa urahisi kwa kutumia kalenda ya simu ya mkononi ambayo itahesabu miaka mirefu (miaka saba ya unabii) baada ya mkataba wa amani wa mpinga Kristo wa Israeli, Yesu Kristo atarudi duniani (Danieli 9:27). Hiyo inawakilisha siku 2,520 (2 x 1260) ama wiki 360 (Ufunuo 11:3, 12:6). Katikati ya dhiki ni wiki 180.

**Maneno ya Yesu (na wengine) kuhusu nyakati za mwisho**

Baadhi ya unabii wa kina wa matukio ya nyakati za mwisho ulizungumzwa na Yesu. Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Yesu akajibu akawaambia, angalieni, mtu asiwadanganye, kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, mimi ni Kristo; nao watawadanganya wengi." (Mathayo 24:4-5). Yesu anazungumza juu ya vita, njaa, matetemeko ya ardhi, manabii wa uwongo, uovu, chuki, na mateso ya waumini, kuhubiriwa kwa injili, na kuchafuliwa kwa hekalu na mpinga Kristo na dhiki kuu na kurudi kwake kwa utakatifu duniani, (Mathayo 24:1-51, 25:1-46, Marko 13:1-37; Luka 17:20-37, 21:5-36; 2Timotheo 3:1-9 [sio maneno ya Yesu]; 2 Petro 3:1-18 [sio maneno ya Yesu]

**Wayahudi 144,000 walioagizwa na Mungu kwa ajili ya utumishi wake**

Malaika wataweka chapa kwenye paji la uso wa watumishi wa Mungu 144,000 ambao utajumuisha jina la mwana kondoo (Yesu) na jina la Baba yake (Mungu). Wayahudi 144,000 kutoka makabila yote 12 ya Israeli wataagizwa na Mungu kwa utumishi wake ambao unaweza kujumuisha uinjilisti. (Ufunuo 7: 1-8, 14:1-5)

**Milenia**

Yesu ataanzisha ufalme wakle wa kidunia ambapo atatawala juu ya watu wote na mataifa ya ulimwengu kwa miaka 1,000. Ufalme wake utajulikana kwa haki na upendo wake wa kweli. Kutakuwa na maelewano katika viumbe vyote wakati dunia inakuwa paradiso yenye kupendeza kama Bustani ya Edeni. Wavulana wadogo watacheza na simba na mbwa mwitu wataishi na mwanakondoo. (Isaya 11:6-9). Watu wataponywa na kuwa na afya njema, wataishi kwa amani na wataongezeka na kuijaza dunia.

Miaka elfu moja itakapokamilika shetani ataachiliwa kutoka kuzimu na atatoka kudanganya mataifa. Wengi watamfuata shetani na kujaribu kumshinda Yesu Kristo. Moto

kutoka mbinguni utawaangamiza na ibilisi atatupwa katika ziwa la kiberiti kinachowaka. Wasiowaumini watahukumiwa mbele ya kiti kikuu cha enzi na kifo na hadesi zitatupwa katika ziwa la moto. (Ufunuo 20). Mbingu ya zamani na dunia ya zamani zitaharibiwa. (2 Petro 3:7, 10:13). Isaya 9:6-7, 11:1-16, 24:23, 35:1-10, 56:1-8, 60:1-22, 61:1-11, 62:1-12, 65:17-25, 66:10-24; Yeremia 31:27-40; Ezekieli 34:11-31, 36:22-38, 37:21-28 sura ya 40-48; Danieli 7:13-14; Yoeli 3:18-21, Amosi 9:11-15, Mika 4:1-8; Habakuki 2:14, Zekaria 8: 1-23, 9:10; Zaburi 2:6-9, 24:7-10, 33:5).

**Mbingu Mpya na Dunia Mpya**

Kufuatia hukumu ya kiti kikuu cha enzi Mungu atafunua mbingu mpya na dunia mpya ambayo haijachafuliwa na dhambi. (Ufunuo, sura ya 21-22, Yohana 14:2-3; 1Wathesalonike 4:17; 2Petro 3:13, Waebrania 12:22-23, Ufunuo 2:7, 7:7-17, 15:2).

"Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu ya kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita wala hapana bahari tena. nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Nasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, tazama masikani ya mungu ni pamoja ya wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maomboleza, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita." (Ufunuo 21:1-4)

"Akaja mmoja wa wale malaika saba… akanionyesha ule mji mtakatifu, Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa mwenyezi Mungu, wenye utukufu wa Mungu, na Mwangaza wake ulikuwa mfano wa kito chenye thamani nyingi kama kito cha yaspi… Na mji ule ulikuwa wa dhahabu safi, mfano wa kioo safi. sikuona hekalu ndani yake; kwa maana Bwana Mungu mwenyezi na mwana-kondoo, ndio hekalu lake. Na mji ule hauhitaji jua wala mwezi kuuangaza, kwa maana utukufu wa Mungu hutia nuru, na taa yake ni mwana-kondoo. Na mataifa yatatembea katika nuru yake. Na wafalme wa nchi huleta utukufu wao ndani yake." (Ufunuo 21:9-26).

"Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu na cha mwana-kondoo; katikati ya njia kuu yake. Na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila

mwezi; na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa. Wala hapatakuwa na laana yoyote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha mwana-kondoo kitakuwamo ndani yake. Na watumwa wake watamtumikia, nao watamuona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao. Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa, wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watawala hata milele na milele." (Ufunuo 22:1-5)

## 6. Tunachoamini

**Biblia**

Tunaamini Biblia ni neno la MUngu na mamlaka ya mwisho katika Imani na Maisha. Kila neno linaongozwa na Mungu, na halina kosa katika maandiko ya awali (2Timotheo 3:16-17, 2 Petro 1:20-21; Mathayo 5:18; Warumi 15:4).

**Mungu**

Tunaamini Mungu mmoja muumba wa vitu vyote, anaishi milele katika nafsi tatu, Baba, Mwana, na Roho mtakatifu. (Mwanzo 1:1, Zaburi 8:1-9, 19:1-4; Warumi 1:20, 8:31-39, 11:33, 2 Wakorintho 13:14; 1 Yohana 4:7-8, Mathayo 28:19-20; Yohana 1:1, 4:24, Yakobo 1:17, Kumbukumbu la Torati 6:4-6; 1 Yohana 4:7-21, 1 Petro 1:13-16; Zaburi 139:1-14, Isaya 45:5, Matendo 17:25)

**Yesu Kristo**

Tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mungu mwana. Kwa kuwa alikuwepo siku zote, alichukua mwili wa kibinadamu na alizaliwa na Bikira Maria. Aliishi maisha makamilifu yasiyo na dhambi duniani. Kifo chake msalabani kililipa adhabu ya dhambi zetu na ndio msingi wa wokovu wetu kwa wale wanaomtumaini. Alifufuka kimwili kutoka kaburini na sasa anatawala na Baba. Yeye ndiye njia pekee ya kwenda kwa Mungu. Tunasubiri kurudi kwake na utukufu wake duniani kudai watu wake na kuhukumu (Yohana 1:1-18, 29, 8:58, 14:6, Luka, sura ya 1-2, 2 Wakorintho 5:20-21, 1 Petro 1: 3-9, Waebrania 1:8, Isaya 7:14, 9:6)

**Roho Mtakatifu**

Tunaamini kuwa Roho Mtakatifu ni Mungu. Anakaa katika muumini, humtukuza Kristo, huongoza, hutuelekeza na kutuwezesha kuishi na Huduma ya Mungu. (Yohana 14:26, 15:26, 16:7-15, Warumi 8:5-18, 26-27; 1 Wakorintho 2:10, 12:12-14; Waefeso 1:13-14)

**Mwanadamu**

Tunaamini kwamba wanadamu waliumbwa kwa mfano wa Mungu lakini walianguka katika dhambi na kwa hivyo wamezaliwa wakiwa wamekufa kiroho na kupotea. Kupitia Imani ya kibinafsi katika Yesu Kristo na kuzaliwa upya kwa roho mtakatifu kunaweza kupatikana maisha ya kiroho na wokovu (Mwanzo 1:26-31, 2:7-25, 3:1-24; Warumi 3:23, 5:12, 6:23).

**Wokovu**

Tunaamini kwamba wokovu ni zawadi ya bure kutoka kwa Mungu mbali na matendo, ilikiwa na wote ambao kwa Imani wanampokea Bwana Yesu Kristo. (Waefeso 1:13-14, 2:8-10, Yohana 1:12, 29, 3:36, 5:24, 14:6, 20:31, 1 Yohana 5:11-13, Matendo 16:31, Warumi 1:16, 5:8, 10:9-10; 2 Wakorintho 5:17, Matendo 4:12, Tito 3: 5-6).

**Ibada (amri)**

Tunaamini kuwa ushirika (chakula cha bwana) na ubatizo wa muumini kwa kuzamishwa unapaswa kusherehekewa (Mathayo 26:26-28; 1 Wakorintho 11:23-26, Mathayo 28:19-20, Matendo 8:26-40).

**Kifo, hukumu, mbingu na kuzimu**

Tunaamini katika ufufuo wa mwili wa wafu; ya muumini kwa baraka ya milele na furaha na bwana, na adhabu ya fahamu kwa makafiri (Luka 14:14, 23:42-43, Yohana 5:28-29, Ufunuo 20:10-15, sura ya 21-22).

## 7. Ukweli kutoka katika biblia

Mungu ndiye chanzo na ukweli wote. Biblia ina mengi ya kusema juu ya ukweli.

- **Zaburi 25: 5,** "Uniongoze katika kweli yako, na kunifundisha, maana wewe ndiwe Mungu wa wokovu wangu, nakungoja wewe mchana kutwa."
- **Zaburi 145:18,** "Bwana yu karibu na wote wamwitao kwa uaminifu."
- **Methali 12:19,** "Mdomo wa kweli utathibitishwa milele, bali ulimi wa uwongo ni wa kitambo tu."
- **Yohana 8:31-32,** "Basi Yesu akawaambia wale wayahudi waliomwamini, nyinyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaeka huru."
- **Yohana 14:15-17,** "Mkinipenda mtashika amri zangu, name nitamwomba Baba, naye atawapa msaidizi mwengine ili akae naye hata milele, ndiye roho wa kweli; ambaye Mungu hauwezi kumpokea kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu."
- **Yohana 16:13,** "Lakini yeye atakapokuja huyo roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake Mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena na mambo yajayo atawapasha habari yake."
- **2 Wathesalonike 2:10,** "…watapotea kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa."
- **3 Yohana 1: 4,** "Sina furaha kuu kuliko hii, kusikia kwamba watoto wangu wanakwenda katika kweli."

**Ni nini maana na kusudi la maisha?**

Baadhi ya maswali muhimu na ya kina katika maisha ni; Mimi ni nani? Nilitoka wapi? Nitaenda wapi nitakapokufa? Kwa nini niko hapa na nini maana na kusudi la maisha? Biblia ina majibu ya maswali haya yote na mengine mengi pia.

- **Kumbukumbu la Torati 6:4-7,** "Sikiza ee Israeli; Bwana Mungu wetu Bwana ndiye mmoja. Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa nguvu zako zote. Na maneno haya ninayo kuamuru leo yatakuwa katika

moyo wako. Nawe uwafundishe watoto wako kwa bidi na kuyanena uketipo katika nyumba yako na utembeapo njiani, na ulalapo na uondokapo.”

- **Wakolosai 3:17,** “Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.”
- **Kutoka 20:3-4, 7-8, 12-17,** “Usiwe na miungu mingine ila mimi. Usijifanyie sanamu ya kuchonga…Usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako…Ikumbuke siku ya sabato na uitakase…Waheshimu Baba yako na mama yako…Usiue…Usizini, Usiibe, Usimshuhudie jirani yako uongo, Usitamani chochote alicho nacho jirani yako.” (amri kumi).
- **Zaburi 23:1-6,** “Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu. Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, kando ya maji ya utulivu huniongoza. Huninuwisha nafsi yangu, pia kuniongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana uwe upo pamoja name, Gongo lako na fimbo yako vyanifariji, waandaa meza mbele yangu, machoni pa watesi wangu. Umenipaka mafuta kichwani pangu, na kikombe changu kinafurika. Hakika wema na fadhili zako zitanifuata siku zote za maisha yangu name nitakaa nyumbani mwa Bwana milele.”
- **1 Wakorintho 13:4-8,** “Upendo huvumilia, hufadhili, upendo hauhusudu, upendo hautakabari, haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahia pamoja na kweli; huvumilia yote, huamini yote, hutumaini yote, hustahimili yote. Upendo haupungui neno wakati wowote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika.”
- **Yeremia 29:11,** “Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala sio ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.” (Mungu anataka umjue, umpende na umtumikie kwa hamu. Mungu ana mpango juu ya maisha yako.)
- **Tito 2:11-14,** “Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na usawa, katika ulimwengu huu wa sasa; tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu; Mungu mkuu na mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi yake kwa

ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema."

- **Mathayo 28:19-20,** "Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote aliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." (Agizo kuu: hili lilikuwa mojawapo ya mambo ya mwisho ambayo Yesu aliwaambia wanafunzi kabla ya kupaa mbinguni.)
- **Marko 12:28-30,** "Na mojawapo wa waandishi akafika akawasikia wakisemezana naye, akatambua ya kuwa amewajibu vema, akamwuliza, katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza? Yesu akamjibu, ya kwanza ndiyo hii, sikia Israeli, Bwana Mungu wetu ni mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na ya pili ndiyo hii, mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi." (Amri Kuu).
- **Yohana 1:12,** "Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake."
- **1 Petro 1:3-9,** "Ahimidiwe Mungu, Bwana wa mabwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu; tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotuzwa mbinguni kwa ajili yenu. Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya Imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa siku ya mwisho. Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali; ili kwamba kujaribiwa kwa Imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo; ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekana kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo. Naye mwampenda, ijapokuwa hamkumuona; ambaye ijapokuwa hamwoni sasa, mnaamini; na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka, yenye utukufu, katika kuupokea mwisho wa Imani yenu, yaani, wokovu waroho zenu."
- **Waefeso 1:3,** "Atukuzwe Mungu, Baba wa Baba wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu waroho, ndani yake Kristo."

- **2 Petro 1:3,** “Kwa kuwa uweza wake wa uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe.”
- **Mwanzo 1:26,** “Mungu akasema, na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.”
- **Yohana 3:16-18,** “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila mtu mwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakuliamini jina la mwana pekee wa Mungu.”
- **Luka 23:43,** “Yesu akamwambia, “Amini, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja name peponi.” (Ukiwa na uhusiano wa kibinafsi na Yesu Kristo, utaenda mbinguni mara moja utakapokufa.)
- **Methali 3:5-6,** “Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako.”
- **Mathayo 6:25-34,** “Kwa sababu hiyo nawambieni, msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini, wala miili yenu mvae nini. Maisha Je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi Je! Si bora kupita hao? Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongezea kimo chake hata mkono mmoja? Na mavazi, ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo, hayafanyi kazi, wala hayasokoti, name nawaambia, ya kwamba hata Suleimani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo. Basi ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo na kesho hutupwa kalibuni, Je! Hatozidi sana kuwavika ninyi, enyi wa Imani haba? Msisumbuke, basi mkisema tule nini? Au tunywe nini? Au tuvae nini? Kwa maana hayo yote mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa. Basi msisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe, yatosha kwa siku maovu yake.”

- **Warumi 15:13,** “Basi Mungu wa Tumaini na awajaze ninyi furaha yote na amani katika kuamini, mpate kuzidi sana kuwa na tumaini, katika nguvu za roho mtakatifu.”
- **Wafilipi 2:3-4,** “Msitende neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu kila mtu amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine.”
- **Wafilipi 4:13,** “Naweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.”
- **Mathayo 17: 20,** “Yesu akawaambia, kwa sababu ya upungufu wa Imani yenu, kwa maana, amin, nawaambia, mkiwa na Imani kiasi cha punji ya haradali mtauambia mlima huu, uondoke hapa uende kule, nao utaondoka; wala halitakuwako neno lisilowezekana kwenu.”

**Unabii uliotimizwa kwa kuja kwa Masihi (Yesu) kwanza**

Neno la Mungu lina unabii mwingi juu ya Masiya. Masihi angekuja akiwa mtoto mchanga na angekuwa mwana wa Mungu. “Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani kwake; naye ataitwa jina lake mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, mfalme wa amani. Maongezi ya enzi yake ya amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake, kuuthibitisha na kuutengeneza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo. Hukumu kwa ujeuri na udhalimu.” (Isaya 9:6-7)

Masihi angezaliwa na bikira na ataitwa Imanueli (ambayo inamaanisha “Mungu pamoja nasi”) “Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina la Imanueli.” (Isaya 7:14).

Masihi huyo angezaliwa Bethlehemu na kuwa mtawala juu ya Israeli. “Bali wewe Bethlehemu Efrata uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda, kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakaye kuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele” (Mika 5:2)

Masihi aliyeteseka alikuwa mwanakondoo wa Mungu ambaye maisha yake yalikuwa sadaka ya dhambi.

**Isaya 52:13-15**

**13.** Tazama mtumishi wangu atatenda kwa busara, atatukuzwa na kuinuliwa juu, naye atakuwa juu sana.

**14.** Kama vile wengi walivyotustaajabia, (uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu yeyote na umbo lake zaidi ya wanadamu.

**15.** Ndivyo atakavyowasitusha mataifa wengi; wafalme watamfumbia vinywa vyao; maana mambo wasiyoambiwa watayaona; na mambo wasiyoyasikia watayafahamu.

**Isaya 53:1-12**

1. Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? Na mkono wa Bwana amefunuliwa nani?
2. Maana alikuwa mbele zake kama mche mwororo, na kama mzizi katika nchi kavu; yeye hana umbo wala uzuri; na tumuonapo hana uzuri hata tumtamani.
3. Alidharauliwa na kukataliwa na watu; mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao; alidharauliwa na wala hatukumhesabu kwa kitu.
4. Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu na kuteswa.
5. Bali aliyejeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maonevu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.
6. Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na Bwana ameweka juu yake makosa yetu sisi sote.
7. Alionewa lakini alinyenyekea, wala hakufunua kinywa chake; kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, na kama vile kondoo anyamazavyo mbele yao wakatao manyoya yake . Naam hakufunua kinywa chake.
8. Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa. Na maisha yake ni nani atakayeisimulia? Maana amekataliwa mbali na nchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu
9. Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; ingawa hakutenda jeuri; wala hapakuwa na hila kinywani mwake.
10. Lakini Bwana aliridhika kumchukua; amemhuzunisha; utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi, ataona uzao wake , ataishi siku nyingi na Mapenzi ya Bwana yatafanikiwa mkononi mwake.

11. Ataona mazao ya taabu ya nafsi yake na kuridhika.  Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki; naye atayachukua maovu yao.
12. Kwa hiyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu, naye atagawanya nyara pamoja nao walio hodari; kwa sababu alimwaga nafsi yake hata kufa akahesabiwa pamoja nao wakosao. Walakini alichukua dhambi za watu wengi na kuwaombea wakosaji.

**Kutimiza unabii wa Kimasihi (uorodheshaji)**

**Unabii wa Agano la Kale…unabii wa Agano Jipya**

- Kizazi cha Ibrahimu (Mwanzo 12:2-3…Mathayo 1:1; Wagalatia 3:16)
- Kizazi cha Yuda (Mwanzo 49:10…Mathayo 1:2)
- Kizazi cha Daudi (Samweli 7:12-16, Yeremia 23:5…Mathayo 1:1)
- Kuzaliwa kwa bikira (Isaya 7:14, Mwanzo 3:15…Mathayo 1:18, 23)
- Kuzaliwa Bethlehemu (Mika 5:2…Mathayo 2:1-12)
- Yeye ni wa milele (Mika 5:2, Isaya 9:6, 53:10-11, Zaburi 110:1…Yohana 1:1, 14, 8:58, Waebrania 1:8)
- Yeye ni mwana wa Mungu (Yeremia 23:6, Isaya 9:6-7…Yohana 20:31)
- Utume wake (Isaya 61:1…Luka 4: 16-21)
- Mjumbe kuandaa njia yake (Isaya 40:3, Malaki 3:1, 4:5-6…Mathayo 3:1-3, 11:7-11)
- Mnyenyekevu na amepanda punda (Zekaria 9:9…Mathayo 21:5)
- Mtu wa amani (Isaya 53:9…Yohana 14:27)
- Mtu wa hekima na ukweli (Isaya 52:13, 53:9, 11…Yohana 14:6)
- Mtu mwenye haki (Isaya 53:11…Luka 23:47)
- Kuinuliwa sana (Isaya 52:13,15, 53:12…Wafilipi 2:9-11)
- Jiwe kuu la pembeni (Isaya 28:16…1 Petro 2:6)
- Mpatanishi wa agano jipya (Yeremia 31:31-34, Isaya 42:6-7, 53:12…Waebrania 12:24)
- Mjumbe wa agano jipya (Malaki 3:1…Mathayo 26:28)
- Mfalme (Nambari 24:17, Yeremia 23:5, Zaburi 2:6…Mathayo 21:5)
- Nabii (Kumbukumbu za torati 18:15-19…Matendo 3:22)
- Makuhani (Zaburi 110:4…Waebrania 5:5-10)
- Alikataliwa (Zaburi 118:22, Isaya 53:3…Mathayo 21:42)

- Aliteseka (Isaya 53:3-4, 5, 7,11...Luka 18:31-33)
- Mateso yake yalileta amani na uponyaji (Isaya 53:5…Matendo 10:36, 1Petro 2:24)
- Mwili ulitobolewa (Zekaria 12:10, Isaya 53:5…Yohana 19:34, 20:25,27)
- Hakuna mifupa iliyovunjika (Zaburi 34:20, Nambari 9:12, Kutoka 12:46…Yohana 19:33-36)
- Kucheza Kamari kwa mavazi yake (Zaburi 22:18...Mathayo 27:35)
- Kuharibiwa kwa sura yake (Isaya 52:14…Yohana 19:1-3, 18)
- Kupigwa mijeledi (Isaya 53:5...Yohana 19:1)
- Kondoo wa Mungu (Isaya 53:7…Yohana 1:29)
- Maisha yake kuwa sadaka ya dhambi (Isaya 53:10…2 Wakorintho 5:21, Warumi 8:3-4)
- Kuleta dhambi ulimwenguni (Isaya 53:4-6,8,11-12…Waebrania 9:28, 1 Petro 2:24)
- Kifo chake (Isaya 53:8-9,12, Danieli 9:25-27, Zekaria 13:7…Yohana 19:18)
- Ufufuo wake (Zaburi 16:10...Mathayo 28:6, Matendo 2:22-36, 13:32-37)
- Kupaa kwake (Zaburi 68:18…Matendo 1:9-11, Waefeso 4:8)

- Masihi Yesu Kristo, "MFALME WA WAFALME NA BWANA WA MABWANA" arudi duniani mwisho wa dhiki kuu kuwaokoa watu wake, kuhukumu waovu na kutawala ufalme wake kidunia. (Ufunuo sura 19-20, Isaya 34:1-17, 66:15-17, Daudi 12:1-13, Joeli 2:28-32, 3:1-17, Zekaria sura ya 12-14, Mathayo 25:31-46, Luka 17:20-37, 2 Wathesalonike 1:1-12, 2:1-12, Tito 2:11-14)

**Malaika**

Malaika ni viumbe wa kiroho walioumbwa na Mungu ili wamtumikie, "Ni roho zinazohudumia zilizotumwa kutumikia wale watakaorithi wokovu." (Waebrania 1:14). Malaika wanawasilisha ujumbe maalum kwa Mungu (Mwanzo 22:11, Waamuzi 13:3-5, Zekaria 2:1-6, Luka 1:11-20, 26-38; Mathayo 28:1-7) wana akili, wana uwezo mkubwa sana na mara nyingi huwalinda na kuwasaidia waumini. (Mwanzo 19:15-17, 48:16, Kutoka 23:20-23, 2Samweli 14:20, 1Wafalme 19:5-7, Matendo 5:19, 12:7-11. Malaika humtumikia Mungu kwa kutekeleza hukumu ya Kimungu. Mwanzo 19:12-13, 2Samweli 24:15-17, 2Mambo ya Nyakati 32:21). Katika nyakati za mwisho, malaika pia watasaidia katika kutekeleza hukumu nyingi. (Mathayo13:40-42, 49-50, 2Wathesalonike 1:6-8, Ufunuo 6:1-17, 8:1-13, 9:1-21, 11:15-19, 15:1-16,21). Malaika mara

nyingi huonyeshwa kama kutoa kutoa heshima na utukufu na sifa kwa Bwana (Zaburi 103:20-21; Ufunuo 5:11-12)

“Nikaona nikasikia sauti ya malaika wengi pande zote za kile kiti cha enzi na za wale wenye uhai na za wale wazee na hesabu yao ilikua elfu kumi mara elfu kumi na elfu mara elfu. Walizunguka kiti cha enzi na viumbe hai na wazee wakisema kwa sauti, astahili mwana-kondoo aliyechinjwa kupokea uwezo na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka!” (Ufunuo 5:11-12).

- **Mathayo 18:10,** “Angalieni msidharau mmojawapo wadogo hawa kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni.”
- **Kutoka 23:20,** “Tazama mimi namtuma malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengenezea.”
- **2 Samweli 24:16,** “Lakini huyo malaika aliponyosha mkono wake kuelekea Yerusalemu ili auharibu, Bwana akaghairi katika mabaya, akamwambia huyo malaika mwenye kuharibu watu, yatosha, sasa ulegeze mkono wako. Naye yule malaika wa Bwana alikuwako karibu na kiwanja cha kupuria cha Arauna Myebusi.”
- **2 Wafalme 19:35,** “Ikawa usiku huo malaika wa Bwana alitoka, akakiingia kituo cha washauri, akawapiga watu mia na themanini na tano elfu. Na watu walipoondoka asubuhi na mapema Kumbe! Hao walikuwa maiti wote.”
- **Luka 2:8-15,** “Na katika nchi ile ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku. Malaika wa Bwana akawatokea ghafla, utukufu wa Bwana ukawang’aria pande zote, wakaingiwa na hofu kuu. Malaika akawaambia, “msiogope kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote. Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa kwa ajili yenu, mwokozi ndiye Kristo Bwana. Na hii ndiyo ishara kwenu, mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto amelala katika hori ya kulia ng’ombe. Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu na kusema, “Atukuzwe Mungu juu mbinguni na duniani iwe amani kwa watu alowaridhia.” Ikawa malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wale wachungaji waliambiana, “Haya na twendeni mpaka Bethlehemu tukalione hilo lililofanyika, alilotujulisha Bwana.”

**Shetani (Ibilisi, Lusifa) na Mapepo**

Agano la Kale na Agano Jipya linaonyesha wazi kuwepo kwa shetani. Shetani anaonekana kwanza katika kitabu cha Mwanzo 3 kama nyoka. Uwepo wake ni maarufu zaidi katika agano jipya. Ibilisi ni malaika aliyeanguka. (Ezekiel 28, Isaya 14) kwa sababu ya dhambi yake (kiburi) alitupwa mbali na uso wa Mungu (Ezekiel 28:16). Mapepo ni malaika walioanguka wavyeo vya chini na wako chini ya mamlaka ya shetani. Shetani na mashetani wake ni viumbe wa roho, wana akili, wana nguvu, wanaweza kuambukiza magonjwa, kuathiri akili, kudanganya watu na hata kudanganya mataifa. (Mathayo 8:16, 12:24, 25:41; Ufunuo 12:7, 16:14; Luka 10:17, 20,13:11, 16, Marko 1:24, 5:3-4; 1Timotheo 4:1, Mwanzo 3:1-5, 1 Wathesalonike 3:5).

- **Yakobo 4:7,** “Basi mtiini Mungu. Mpingeni shetani, naye atawakimbia.”
- **1 Petro 5:8-9,** “Muwe na kiasi na kukesha kwa kuwa mshitaki wenu ibilisi, kama simba anguramaye huzunguka-zunguka akitafuta mtu ammeze. Nanyi mpingeni huyo mkiwa thabiti katika Imani mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani.”
- **2 Wakorintho 11:14,** “Wala si ajabu maana shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru.”
- **Ufunuo 20:10,** “Na yule ibilisi mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti, alimo yule mnyama na yule nabii wa uongo. Nao watateswa mchana na usiku hata milele na milele. Wafu wakuhukumiwa.”

## 8. Mambo ya kimsingi kutoka kwenye biblia

### Utangulizi wa Biblia

Biblia ni neno la Mungu na mamlaka ya mwisho katika Imani na maisha. Kila neno linaongozwa na Mungu na halina kosa katika maandiko ya awali (2 Timotheo 3:16-17, 2 Petero 1:20-21, Mathayo 5:18, Warumi 15:4).

“Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, yafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao na kuwaongoza na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.” (2 Timotheo 3:16-17)

Biblia ni ya kipekee. Iliandikwa na waandishi zaidi ya 40 tofauti kutoka Nyanja mbalimbali za kimaisha kwa kipindi cha takribani miaka 1,500. Vitabu sitini na sita vya Biblia viliandikwa kwa lugha tatu tofauti (Kiebrania, Kiaramu na Kiyunani) katika mabara matatu tofauti (Asia, Afrika na Ulaya). Biblia inafafanua Mungu ni nani, jinsi tunavyoweza kuokolewa na jinsi tunavyoweza kumtukuza Mungu katika mawazo yetu, maneno na matendo yetu. Imegawanywa katika Agano la Kale na Agano Jipya.

Agano la kale lina vitabu thelathini na tisa vinavyoelezea juu ya uumbaji wa ulimwengu na mwanadamu, kuanguka (dhambi) kwa mwanadamu, mafuriko, maisha ya Ibrahimu, Isaka na Yakobo, kukombolewa kwa watu wa Mungu kutoka utumwani Misri, kuzaliwa kwa taifa la Israeli, kutolewa kwa sheria kwenye mlima Sinai, ushindi wa Kanaani (nchi ya ahadi), kipindi cha waamuzi, wafalme wa kwanza (Sauli, Daudi na Suleimani), hekalu la kwanza (Suleimani), mgawanyiko wa Israeli katika ufalme wa kaskazini (Israeli) na ufalme wa kusini (Yuda), utekwaji wa Israeli na Waashuri, kuharibiwa kwa hekalu na utekaji wa Yuda na Wababeli. Kurudi kwa Yuda Yerusalemu na kuwekwa wakfu kwa hekalu la pili (Zembabeli). Agano nyingi za zamani huzingatia kushughulika kwa Mungu na watu wa Israeli kwa msingi wa agano alilofanya nao kwenye mlima Sinai. Katika Agano lote la Kale kuna msitari wa unabii kuhusu mwokozi anayekuja, Masihi wa taasis za Agano Jipya. Utimilifu wa unabii huu ni hadithi ya Agano Jipya. Kuna kipindi cha miaka 400 kati ya nabii wa mwisho wa Agano la Kale, Malaki, na kuzaliwa kwa Masihi (Yesu).

Agano Jipya lina vitabu ishirini na saba ambavyo viliandikwa kutoka karibu 35 baada ya Kristo hadi 95 baada ya Kristo. Agano Jipya linaelezea uhusiano wa Mungu na wanadamu kupitia Masihi kwa msingi wa agano jipya. (Yeremia 31:31-34, Luka 22:14-20, 2Wakorintho 3:6-11) Agano la Kale lilionyesha utakatifu wa Mungu katika kiwango cha haki cha sheria na mkombozi aliyeahiwa; Agano Jipya linaonyesha utakatifu wa Mungu katika mwanawe mwenye haki (Yesu). Agano Jipya basi lina maandishi hayo ambayo yanafunua yaliyomo ikiwa ni Agano Jipya. Ujumbe wa Agano Jipya unazunguka kwa masihi ambaye alitoa maisha yake kama sadaka ya dhambi (Isaya 53:10; Mathayo 26:28) na watu (Kanisa) waliopokea wokovu. Kwa hiyo mada kuu ya Agano Jipya ni wokovu. Injili inamtambulisha mwokozi (Yesu). Kitabu cha Matendo kinaelezea kuenea kwa habari njema juu ya wokovu wake. Agano Jipya lote linatoa maelezo ya baraka za wokovu huo.

**Vitabu vya Agano Jipya vya Biblia**

**Kichwa cha kitabu-mada-mistari inayosaidia**

**Vitabu vinne vya Injili na Matendo-**Maisha ya Kristo, kuzaliwa kwa kanisa, Mateso ya Wakristo, Kueneza Ukristo

- **Mathayo –** Yesu Mfalme- Kuzaliwa 1-2, ubatizo 3, mahubiri ya mlimani 5-7, sala 6:5-13, wasiwasi 6:25-34, nyakati za mwisho 24-25, kusulubiwa 27:27:66, Ufufuo 28:1-10, Agizo kuu 28:19-20.
- **Marko –** Mtumishi 10:45, Nyakati za mwisho 13, kusulubiwa 15:21-47, ufufuo 16:1-8.
- **Luka –** Yesu mwana wa binadamu – 19:10, 24:46-48, Kuzaliwa 1-2, Ubatizo 3:1-22, upendo wa dhati 6:27-38, Nyakati za mwisho 17: 20-37, 21:5-36, SKusulubiwa 23:26-56, Ufufuo 24:1-12.
- **Yohana –** Yesu mwana wa Mungu – 20:31, hapo mwanzo 1:1-18, ubatizo 1:19-34, kusulubiwa 19:17-42; Ufufuo 20:1-18.
- **Matendo –** Kuzaliwa, ukuaji na mateso ya kanisa 1:1-11, kuzaliwa kwa kanisa 2, kuanza kwa mateso 4, Stefano, muumini wa kwanza kuuawa 6:8-8:3. Uongofu wa Paulo 9:1-31, Uongofu wa mataifa 9:32-10:48, Kukamatwa kwa Paulo 21:27-22:29.

**Vitabu vya Mtume Paulo**

- **Warumi –** Wokovu kwa Imani-ghadhabu ya Mungu 1:16-32, haki 3:21-31, 5:1-21,endelea kutenda dhambi6, wema wa Mungu 8:26-39, Wokovu kwa Imani 10:1-17, kufanya upili akili yako 12:1-18.
- **1 Wakorintho –** marekebisho 6:19-20, ndoa 7, majaribu 10:12-13, 31, Zawadi za kiroho 12:1-14:40, upendo unaofafanuliwa 10: 1-13, Injili imeainishwa 15:1-5, unyakuo 15:51-58, Kutoa 16:2
- **2 Wakorintho –**Huduma ya Kikristo 4:16-18, 13:5, 14 uhakika wa ufufuo 5:1-9, kiti cha ukumu cha Kristo 5:10-13, Upendo wa Kristo 5:14-21, Kutoa 8:1-9:15, Maono ya Paulo 12:1-10.
- **Wagalatia -** Uhuru wa sheria – Wokovu kwa Imani 2:16-4:31, Uhuru 5:1-15, Matunda ya roho 5:16-26, Ndugu mwenye dhambi 6:1-5.
- **Waefeso –** Kujenga mwili wa Kristo – Waliochaguliwa na kutiwa chapa 1:3-23, kuokolewa kwa neema 2:1-10, mwili wa Kristo 2:11-4:6, karama za kiroho 4:7-16, mazoezi ya waumini 4:17-6:9, ndoa na familia 5:22-6:4, kuwa imara katika Imani 6:10-20.
- **Wafilipi –** Kuishi na Kristo – 1:6,21, 3:8, Unyenyekevu 2:1-18, wasiwasi 4:6-8, amani kwa hali 4:10-23.
- **Wakolosai –** Ukuu na utoshelevu wa Kristo - Tabia ya Kristo 1:15-23, agizo kuu kwa Paulo 1:24-29, Ukristo ulioinuliwa 2, wito mkuu 3:1-4:6, maisha ya familia 3:18-21.
- **1 Wathesalonike –** Utakatifu wakati wa kungojea kuja kwa Kristo – Ukuaji katika bwana 3:9-13, nyakati za unyakuo wa mwisho 4:13-5:11, furahi, Sali, Toa shukrani 5:16-18
- **2 Wathesalonike –** Udhabiti wakati wa kungojea kuja kwa Kristo, Hukumu ya mwisho na unafuu 1:3-12, Uasi sheria wa binadamu 2:1-13, Simama imara 2:13-17.
- **1 Timotheo –** Mwongozo wa uongozi na tabiakanisani – 1:5-6, maagizo juu ya ibada 2:1-15, wajane na wakuu 5:1-25, Pesa na Uungu 6:6-19.
- **2 Timotheo –** Huduma ya uvumilivu 1:7, 3:16-17, Ujasiri na uaminifu 1:8-18, wanajeshi la Kristo 2:1-26, Siku za mwisho 3:1-9, Mateso 3:10-15, taji ya haki 4:6-8.

- **Tito –** Mwongozo wa kufanya- Wazee kanisani 1:5-9, Neema 2:11-15, kuokolewa kwa neema 3:5-7.
- **Filemoni –** Msamaha – Ombi la Paulo kwa Onesimo 1:8-21

**Vitabu vilivyoandikwa na Petro, Yohana, Yakobo na wengine**

- **Waebrania –** Ukuu wa Kristo -4:12, 12:1-2, Kuhani Melkizedeki na Agano Jipya 7:1-8:13, Agano la kwanza na Agano Jipya 9:1-10:31, Imani iliyofafanuliwa 11.
- **Yakobo –** Imani inayofanya kazi – Majaribu 1:2-18, kusikiliza na kutenda 1:19-27, Imani na matendo 2:14-26, kuzuia ulimi 3:1-12, Hekima ya kweli 3:13-18, ulimwengu 4.
- **1 Petro –** Kuteseka kwa ajili ya Kristo – tumaini lililo hai 1:3-12, kuwa watakatifu 1:13-25, ndoa 3:1-7, kuteseka 3:13-4:19, unyenyekevu na wasiwasi 5:5-7.
- **2 Petro –** Dhidi ya walimu wa uongo – wito wa mtu na uchaguzi 1:3-11, unabii wa maandiko 1:12-21, Walimu wa uongo 2, Nyakati za mwisho 3
- **1 Yohana –** Ushirika – Sifa za ushirika 2:28-3:24, maonyo ya ushirika 4, matokeo ya ushirika 5.
- **2 Yohana –** Epuka walimu wa uongo – Pendaneni 1:5-6, walimu wa uongo 1:7-11.
- **3 Yohana –** Ushirika na watoto wa Mungu, ushawishi wa Gayo 1:2-8.
- **Yuda –** Shindania Imani – dhambi na hukumu ya watu wasiomcha Mungu 1:3-16, kuvumilia wito 1:17-23.
- **Ufunuo –** Ufunuo wa Yesu Kristo – Ujumbe kwa makanisa saba 2:1-3:22, chapa wa hukumu 6, Wayahudi 144000 7:1-8, 14:1-5, hukumu ya paragumu 8:1-9:21, 11:15-19, mashahidi wawili (manabii) 11, Vita duniani na mbinguni 12, mnyama na nabii wa uongo 13, Hukumu ya bakuli 15-16, Babeli mkuu 17-18, Kristo arudi duniani 19, Milenia 20,Mbingu mpya, dunia mpya, Yerusalemu mpya 21:1-22:5, epilogi 22:6-21.

**Vitabu vya Agano la Kale la Biblia**

**Kichwa cha kitabu – Mada – Vifungu muhimu**

**Vitabu vitano vya Musa (Sheria)**

- **Mwanzo –** Mwanzo – Mwanzo wa uumbaji 1-2, Anguko 3:1-24, Nuhu na mafuriko 6-9, mnara wa Babeli 11:1-9, Historia ya Ibrahimu 11:27-25:11, wito wa Ibrahimu 12:1-9,

Agano la Bwana na Abramu 15:1-21, historia ya Isaka 21-25, Yakobo na Esau 25:19-36:43, wana kumi na wawili wa Yakobo 29 - 50, historia ya Yusufu 37 – 50.

- **Kutoka –** Ukombozi kutoka Misri – Israeli huko Misri; Utumwa 1:1-12:36, Maandalizi na wito wa Musa 2-4, Mungu amtuma Musa kwa Farao 5:1-7:13, mapigo 7:14-12:36, Pasaka ya kwanza 12:1-36, kuondoka Misri 12:37-51, safari ya Israeli kwenda Sinai 12:37-18:27, utoaji wa sheria 19-24, maskani 25-31, 35-40, uvunjaji wa sheria 32-34.
- **Mambo ya walawi –** Utakatifu, sadaka 1-17, utakaso 18-27.
- **Hesabu** – Waisraeli wanalalamika 11-12, Wapelelezi wa Kanaani 13, Israeli waasi 14, Nidhamu kutoka kwa Mungu 15-20.
- **Kumbukumbu la Torati –** Agano-Amri kumi za Mungu 5:6-21, mpango 6:4-9, ahadi ya baraka na laana 28, Agano la Palestina 29-30, kifo cha Musa 34.

**Vitabu vya kihistoria –vitabu kumi na viwili**

- **Yoshua –** Mkutano na mgawanyiko – 1:8-9, kuingia katika nchi ya Kanaani 1-5, kushinda nchi ya Kanaani 6-12, kuigawanya nchi ya Kanaani 13-24.
- **Waamuzi –** Mizunguko, Debora na Baraka 4-5, Ukombozi wa Gideoni 6-8, Yeftha 10:6-12:7, Samsoni 13-16.
- **Ruthu –** Jamaa- mkombozi- kujitolea kwa Ruthu 1:16-17, Boazi kama jamaa-mkombozi 2-4.
- **1 Samweli –** Samweli, Saulo, Daudi – Samweli jaji wa mwisho 1-8, Saulo, mfalme wa kwanza wa Israeli 9-31, Daudi alichaguliwa 16, Daudi anashinda Goliathi 17, Kuinuka kwa Daudi juu ya Sauli 17-31.
- **2 Samweli –** Daudi – Daudi anakuwa mfalme juu ya Israeli 5, dhambi ya Daudi 11, Uasi wa Absalomu 14-18.
- **1 Wafalme –** Mgawanyiko wa ufalme, Suleimani anakuwa mfalme wa Israeli 1:1-3:1, Hekima ya Suleimani, Utawala wa Umaarufu 3:2-4:34, 9:1-9, Hekalu la Suleimani 5-8, kuanguka kwa Suleimani 11, ufalme uligawanyika (Israeli na Yuda) 12-22, Eliya 17-19, 21.

- **2 Wafalme –** Kupungua kwa utumwa wa Israeli na Yuda -  Ufalme uliogawanyika 1-17, Elisha 2-9, Ashuru yashinda Israeli, uhamisho 17, utawala wa Hezekia 18-20, Babeli yashinda Yuda (ametengwa) na kuharibu Hekalu 24-25.
- **1 Mambo ya Nyakati –** Utawala wa mfalme Daudi – upako wa Daudi na utawala 10-29, Suleimani anakuwa mfalme na kifo cha Mfalme Daudi 29:22-30.
- **2 Mambo ya Nyakati –** Maoni ya kikuhani ya Yuda 7:14, 16:9, utawala wa Suleimani 1-9, maombi ya Suleimani kwa hekima 1:7-12, kuwekwa wakfu kwa hekalu la Suleimani 5-7, Wafalme wa Yuda 10-36.
- **Ezra –** Hekalu- Yuda anarudi chini ya Zerubabeli 1-6, ujenzi wa Hekalu (pili) 3-6, kurudi chini ya Ezra 7-10.
- **Nehemia –** Ukuta wa Yerusalemu – Kujenga upya kuta chini ya Nehemia 1-7, kuifany upya agano chini ya Ezra 8-10.
- **Esta –** Utoaji 4:14, Ugunduzi wa Esta 2:1-20, Kujitolea kwa Modekai 2:21-23, Amri ya Hamani 3, watu wa Mungu wakombolewa 6-10.

**Vitabu vya Mashairi – Vitabu vitano**

- **Ayubu –** Enzi kuu – maafa ya Ayubu 1-2, Mijadala ya Ayubu 3-37, ukombozi wa Ayubu 38-42.
- **Zaburi  -** Ibada – Sura kuu 1,22,23,24,37,72,100,119,121, na 150.
- **Mithali –** Hekima – 2:6, 3:5-6, 8:13, 9:10, 15:1, 17:22, 22:6, 23:7, 27:17 kusudi la Mithali 1:1-7, Mithali ya ujana 1:8-9:18, Mithali ya Suleimani 10-29, mke wa maadili mema 31:10-31.
- **Mhubiri –** Ubatili – Yote ni ubatili 1:1-3, Furahia maisha, ni zawadi kutoka kwa Mungu 3:12-13, 3:22, 5:18-19, 8:15, 9:7-9, Mcheni Mungu na mshike amri zake 12:13-14.
- **Wimbo wa Suleimani –** Upendo – Uchumba 1-3, Suleimani amsifu bibi arusi wake 4:1-15, upanuaji wa upendo 5:2-8:14

**Vitabu vya Unabii – Vitabu kumi na saba**

- **Isaya –** wokovu – unabii wa hukumu 1-39, mateso na ushindi wa Masihi 52:13-53:12, unabii wa faraja 40-66.

- **Yeremia –** Saa ya mwisho ya Yuda – wito wa Yeremia 1, agano jipya 31:31-34, unabii kwa Yuda 2-45, unabii kwa mataifa 46-51, kuanguka kwa Yerusalemu 52.
- **Maombolezo –** Maombolezo – Uharibifu wa Yerusalemu 1, Hasira ya Mungu 2, Maombi ya Rehema 3, Kuzingirwa kwa Yerusalemu 4, sala ya marejesho 5.
- **Ezekieli –** Marejesho ya Israeli, tume ya Ezekieli 1-3, Hukumu ya Yuda 4-24, Hukumu ya mataifa 25-32, marejesho ya Israeli 33-48.
- **Danieli –** Mpango wa Mungu kwa Israeli – Historia ya Danieli 1, Tanuru ya moto 3, Tundu la simba 6, mpango wa kinabii wa watu wa mataifa 2-7, unabii wa wiki 9, mpango wa kinabii wa Israeli 8-12.
- **Hosea –** Upendo mwaminifu wa Mungu kwa Israeli – mzinzi na mume mwaminifu 1-3, Israeli mzinzi na Bwana mwaminifu 4-14.
- **Yoeli –** Siku ya Bwana – ukiwa 1:2-2:17, Ukombozi 2:18-3:21.
- **Amosi –** Hukumu ya Israeli – unabii wa Amosi 1:3-2:16, Mahubiri ya Amosi 3-6, maono ya Amosi 7-9.
- **Obadia –** Hukumu ya Edomu 1:1-18, marejesho ya Israeli 1:19-21.
- **Yona –** Uamsho katika Ninawi – tume ya kwanza ya Yuda 1-2, samaki mkubwa anammeza Yuda 1:17, agizo la pili la Yona 3-4.
- **Mika –** Hukumu na urejesho wa Juda- 6:8, utabiri wa hukumu 1-3, utabiri wa urejesho 4-5, ombi la toba 6-7.
- **Nahumu –** Hukumu ya Ninawi – Hukumu ya Ninawi imepungua 1, Uharibifu wa Ninawi umefafanuliwa 2, uharibifu wa Ninawi unastahili 3.
- **Habakuki –** Imani – Shida za Habakuki 1-2, Sifa za Habakuki 3.
- **Sefania –** Hukumu na urejesho katika siku ya Bwana – unabii wa Hukumu 1:2-3:8, unabii wa baraka 3:9-20.
- **Hagai –** Ujenzi wa Hekalu – wito wa ujenzi wa Hekalu (pili) 1, Utukufu wa Hekalu la mwisho 2:1-9, Baraka za sasa za utii 2:10-19, Baraka za badaye za Ahadi 2:20-23.
- **Zekaria –** Maandalizi ya Masihi – wito kwa Toba 1:1-6, Maono ya Zekaria 1:7-6:15, Mizigo inayohusu siku zijazo 9-14.
- **Malaki –** Rufaa kwa wageukao – Huruma ya Mungu kwa Israeli 1:1-5, Malalamiko ya Mungu dhidi ya Israeli 1:6 – 3:15, Hukumu ya Mungu kwa watu 3:16 – 4:6.

**Mpangilio wa Biblia**

- Mungu aliumba Mbingu na nchi Mwanzo 1-2
- Kuanguka (dhambi) kwa mwanadamu, Mwanzo 3
- Nuhu na mafuriko, Mwanzo 6-9
- Ibrahimu, Isaka, Yakobo, na Yusufu, Mwanzo 11-50
- Ukombozi wa watu wa Mungu kutoka utumwani Misri, Kutoka 1-12
- Kuzaliwa kwa taifa la Israeli, Kutoka 12
- Kutoa sheria juu ya mlima Sinai. Kutoka 19-24
- Ushindi wa Kanaani (Nchi ya Ahadi) Yoshua 6-12
- Kipindi cha Waamuzi katika Israeli, Waamuzi 1-21, 1Samweli 1-9
- Samweli, jaji wa mwisho, 1 Samweli 1-25
- Mfalme Sauli (mfalme wa kwanza) aanza utawala wake, 1 Samweli 10
- Mfalme Daudi anaanza utawala wake, 2 Samweli 1-5
- Mfalme Suleiman aanza utawala wake, 1 Wafalme 1-3
- Hekalu la kwanza (la Suleimani) lililowekwa wakfu huko Yerusalemu, 1 Wafalme 8
- Kipindi cha manabii, Isaya hadi Malaki
- Israeli iligawanyika (Israeli kaskazini, Yuda kusini) 1 Wafalme 12
- Utumwa wa Israeli na Waasheri, 2 Wafalme 17
- Uharibifu wa Hekalu na utekwaji wa Yuda na Wababeli, 2 Wafalme 24-25
- Kurudi kwa Yuda Yerusalemu, Ezra 1-10
- Hekalu la pili (Zerubabeli) lililowekwa wakfu, Ezra 6
- Malaki, nabii wa Agano la Kale, Malaki 1-4
- Masihi (Yesu) aliyezaliwa Bethlehemu, Mathayo 2:1-12
- Yesu alisulubiwa, akazikwa na kufufuka , Yohana 19:18, 20:1-18
- Kuzaliwa kwa kanisa (Pentekoste), Matendo 2
- Kuenea kwa Ukristo, Matendo 3-28.

## 9. Rasilimali zinazopendekezwa

### Wokovu na ukuaji wa kiroho

www.billygraham.org **-** Tazama: “Jinsi ya kumjua Yesu.”

www.cru.org **-** Tazama: “Jinsi ya kumjua Mungu.”

### Kujifunza Biblia na utafiti

www.biblehub.com **-** Somo la kusoma Biblia.

www.biblegateway.com – Kujifunza Biblia na utafiti

www.blueletterbible.org – Zana za kujifunza Biblia.

## 10. Maono na Malengo

### Maono

Maono yetu ni kuona mamilioni ya watu wameokolewa na Bwana Yesu Kristo, katika siku kabla na baada ya kunyakuliwa na kuandaa, kusaidia, na kuwaombea wale waliobaki nyuma.

### Malengo

Oparesheni ya uokoaji kutoka kwa dhiki hutumia aina nyingi ya vyombo vya habari ili kushiriki habari njema za Yesu Kristo na ulimwengu wote kabla na baada ya unyakuo. Tumejitolea kuwapa walioachwa nyuma rasilimali zote wanazohitaji kuzindua uamsho mkubwa katika historia ya wanadamu kwa heshima na utukufu wa Bwana Yesu Kristo. Tunatambua tu kwamba njia bora zaidi ya uinjilisti ni uso kwa uso na neno la mdomo…wote waliioga katika sala.

## 11. Kuhusu Sisi

Baada ya kuhisi wito wa kuwasaidia wale ambao wangeachwa nyuma, operesheni ya ukuaji kutoka kwa dhiki (OTR)! Ilizinduliwa mnamo Novemba 2010. Ni muhimu kwamba tuwaonye watu juu ya kurudi kwa Yesu, kuwawezesha wale walioachwa nyuma kuinjilisha (shiriki habari njema ya Yesu Kristo). Wavuti ya www.tribulation rescue.com ni mojawapo ya magari mengi ambayo hutumiwa na OTR kufanikisha dhamira yetu. Hutaona tarehe ya kurudi kwa Bwana iliyowekwa kwenye tovuti hii. Biblia inasema wazi, "Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake." (Mathayo 24:36). Baada ya unyakuu lazima tuonye watu kwamba Yesu anakuja tena duniani. Basi haitakuwa siri. Biblia inatuambia kwamba Yesu atarudi miaka saba ya kinabii (siku 2520; Ufunuo 11:2-3, 12:6) baada ya kutiwa saini kwa mkataba wa amani wa Israeli na mpinga Kristo. Kuwa tayari.

OTR haikubali michango. Shirika hili linaendeshwa kabisa na kikosi cha kujitolea. Ikiwa ungependa kujiunga na timu ya uokoaji kutoka kwa dhiki, tafadhali nenda "kuwasiliana nasi/ jiunge nasi." Lengo letu ni kuwa na wanachama wa timu ya kuwaokoa kutoka kwa dhiki katika kila taifa la dunia. Tafadhali ombea Huduma hii na kwa wale watakaobaki (au walio) nyuma.

**Msingi**

Watu wengi hawaelewi kabisa unyakuo ni nini, Ni kurudi tu kwa Yesu Kristo kuwachukua waumini wake wote kwenda mbinguni kabla ya dhiki kuu ya miaka saba kuanza. Baada ya unyakuu, kutakuwa na watu zaidi ya bilioni sita walioachwa nyuma na wataogopa, kuchanganyikiwa na kutafuta majibu. Wengi wataenda kwenye mtandao na vyanzo vingine kujaribu kuelewa yote na watadanganywa na mafundisho ya uwongo. Kwa bahati mbaya tovuti nyingi za kanisa na huduma ya Kikristo hazitoi habari mahsusi kwa wale walioachwa nyuma. Nadharia nyingi zitapendekezwa kuelezea kilichotokea kwa mamilioni waliotoweka. Udanganyifu wenye nguvu utaanguka juu ya mioyo na akili za wale walioachwa nyuma. "Waamini uongo" (2 Wathesalonike 2:11). Yesu aliwaonya wale wa mwishoni mwa zama , "Angalieni mtu asiwadanganye, kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema mimi ni

Masihi; nao watadanganya wengi.” (Mathayo 24:4-5) Kwa shukrani, neno la Mungu, maombi, upendo wa Kristo na ushuhuda wa unabii uliotimizwa utaweza kukata unabii huo.

Tunatambua kwamba watu wengi hawatasikiliza onyo kwamba Yesu anarudi. Ilikuwa hivyo hivyo katika siku za Nuhu. (Mathayo 24:37-39). Sehemu ya dhamira yetu ni kupanda mbegu sasa kwamba Mungu anaweza kusababisha kulipuka kwa kulipuka kufuatia unyakuo na wakati wa dhiki kuu. Ni maombi yetu kwamba mamilioni ya watu wamtumaini Kristo wakati wa dhiki kuu. Ikiwa ni asilimia tano tu ya watu bilioni sita wanaokolewa ambayo inawakilisha watu milioni 300. Bwana akipenda zaidi ya hawa wataokolewa kwa sababu tunajua kwamba Bwana hataki, “hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikie toba.” (2 Petro 3:9)

Nyakati ngumu ziko mbele kwa wale walioachwa nyuma, “kwa wakati huo kutakuwepo dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe. Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingeokoka mtu yeyote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo.” (Mathayo 24:21-22) Tunaomba kwamba Mungu atafanya kazi kwa njia kuu siku hizi za mwisho na kwamba timu ya uokoaji kutoka kwa dhiki itashiriki katika mlipuko huu wa uinjilisti wa wakati wa mwisho na uamshomkubwa katika historia ya binadamu. Tunaomba kwa bidi hata sasa kwa wale watakaobaki nyuma. Ikiwa unasoma hii baada ya unyakuo, hauko peke yako. Yesu alisema, “Na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” (Mathayo 28:20). Unaweza kuwa na hakika kuwa wewe uko katika maombi yetu. “Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uwezo wa nguvu zake.” (Waefeso 6:10)

## 12. Wasiliana / Jiunge nasi

Kwa habari zaidi kuhusu uokoaji wa dhiki ya operesheni, tafadhali jisikie huru kuwasiliana nasi kupitia barua pepe **mail@tribulationrescue.com**

Je! Ungependa kuwa mwanachama rasmi wa Timu ya Uokoaji wa Dhiki? Baada ya kutimiza mahitaji yafuatayo utakuwa mwanachama rasmi.

1. Lazima uwe muumini katika Bwana Yesu Kristo. Ikiwa wewe si muumini au hauna uhakika, nenda kwa **Jinsi gani naweza kuokoka?** na uokoke. “Mwamini Bwana Yesu nawe utaokoka.” (Matendo 16:31)

2. Ombea Huduma hii na kwa wale ambao watakuwa (au) wameachwa nyuma.
3. Enenza habari kutoka / kuhusu tovuti hii na angalau watu wengine kumi.

Ikiwa umetimiza mahitaji haya matatu, hongera! Wewe sasa ni mwanachama rasmi wa Timu ya Uokoaji wa Dhiki!

Tungependa kusikia kutoka kwako. **Tutumie barua pepe.**

**Ilani!** Kwa sababu za kiusalama, usitutumie jina lako halisi.

**Tutumie**

- Jina la kwanza (lisiwe jina lako halisi)
- Barua pepe
- Mji
- Jimbo (ikiwezekana)
- Nchi

Ikiwa wasoma hii baada ya unyakuo, mwanzoni shirika hili halitawekwa rasmi. Hata hivyo, tumekuwa tukiomba kwamba Mungu atawainua watu ambao wataendelea na maono na dhamira ya operesheni ya uokoaji wa Dhiki.